**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 9 Februari, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 110

**Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji**

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI** aliuliza:-

Kwa kuwa Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji ni tegemeo letu kubwa katika Halmashauri zetu; na kwa kuwa viongozi hao wanapewa madaraka makubwa kupita kiasi, yakiwemo na yale ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao na pia kuwa Mahakimu wa matatizo ya jamii inayowazunguka na wakati mwingine maisha yao kuwa hatarini:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea posho ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kuongeza tija bila kutoboa mifuko yao kwa kile kiasi kidogo cha mshahara wapatacho?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia usafiri angalau wa pikipiki ili kuwaondolea adha ya kutembea mwendo mrefu kwa miguu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji, wameajiriwa na Halmashauri. Maafisa hawa wanalipwa mishahara yao, pamoja na posho mbalimbali kama vile malipo ya uhamisho, safari nje ya kituo cha kazi na likizo. Wakurugenzi wa Halmashauri wanawajibika kuwapatia vitendea kazi, ofisi na kujenga mazingira mazuri

ili wafanye kazi zao kwa ufanisi. Aidha, ni jukumu la Halmashauri, kuhakikisha kuwa, Watendaji hawa wanapata stahili zao.

Mheshimiwa Spika, posho mbalimbali kwa watumishi wa Serikali, zilikwishafutwa na kujumuishwa kwenye mishahara. Napenda kuwashauri Watendaji hawa, wajisomee na kufanya mitihani ili waweze kupanda ngazi na kupata maslahi ya juu, kulingana na muundo wa utumishi wa kada yao. Vilevile napenda kuziagiza Halmashauri, kujenga mazingira mazuri kwa watumishi ili wapende kufanya kazi katika maeneo yao. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, inatoa samani na vifaa vya kupikia kwa watumishi wanaokwenda kuanza kazi katika Halmashauri hiyo. Kwa hiyo, Halmashauri nyingine zinashauriwa ziige mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ili kuwavutia watumishi wakafanye kazi katika Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ni Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, ambapo kwa mwaka huu, imewakopesha pikipiki Watendaji wa Kata katika Kata zote 28. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuwapatia usafiri Watendaji wa Kata na Vijiji. Jukumu hili ni la Halmashauri husika. Napenda kuziagiza Halmashauri kulingana na uwezo, kutumia fursa mbalimbali zilizopo na kupanga mikakati ya kuwapatia usafiri Maafisa Watendaji wa Vijiji na Maafisa Watendaji Kata ili wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi. Pamoja na ufinyu wa bajeti, lakini hata kwa mwaka, Halmashauri ikiamua kununua pikipiki mbili, angalau kwa muda tatizo hili litakuwa limepungua.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

La kwanza, Watendaji wa Kata kama nilivyouliza katika swali la msingi, wamekuwa kama Mahakimu na wamekuwa kama wafanyakazi wa ulinzi na usalama wa raia. Wakiwa vijijini hufanya kazi hizo kwa kuwahangaikia wananchi, kwa kuamua kesi mbalimbali na hatimaye kubeba wahalifu kuwapeleka katika maeneo husika, mfano Makao Makuu ya Wilaya, ambako kuna Vituo vya Polisi.

Watendaji hao, huchukua fedha zao za mifukoni, lakini wanapofika kule, hakuna anayewalipa zile fedha zao ambazo wanakuwa wamezitumia. Wakienda Vituo vya Polisi, hawalipwi na wakienda kwenye Halmashauri hawalipwi. Je, hayo malipo yao ya gharama na fedha zao ambazo wanakuwa wamezitumia, kwa kazi ambazo zimepangwa kimsingi kutoka ngazi za juu na bila malipo nani atawalipa? *(Makofi)*

La pili, naomba kupata jibu endapo Ofisi ya Waziri itawaongezea posho. Ninachozungumzia ni zile fedha ambazo wao wanakuwa wamezitumia nje ya kazi zao. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria, mfanyakazi yeyote akifanya kazi nje ya kituo cha kazi, anatakiwa kulipwa posho ya kujikimu. Mheshimiwa Mbunge, kama kuna mtumishi ambaye amefanya kazi, aidha Mtendaji wa Kata au Mtendaji wa Kijiji, bila kulipwa posho ya kujikimu, nadhani hilo ni tatizo la

Halmashauri husika. Kama wapo Watendaji ambao hawajalipwa posho zao kwa mujibu wa Sheria, naomba hilo alifikishe kwenye Halmashauri husika ili waweze kulipwa posho zao kwa Mujibu wa Sheria. Kwa sababu wanapompeleka mtuhumiwa Mahakamani au sehemu yoyote, wanakwenda nje ya kituo cha kazi, kwa hiyo, wanatakiwa walipwe kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba, hao watendaji wa vijiji na wa Kata wapewe posho maalum. Kwa kweli kwa sasa hivi Serikali haina mpango wa kutoa posho maalum kwa wafanyakazi wote, ila kwa sasa Serikali inachofanya ni kuangalia upya mishahara ya wafanyakazi wote bila kubangua.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa wote tunakubali kwamba Watendaji angalau wa Kata ni *engine* ya maendeleo katika nchi yetu; na kwa kuwa sasa hivi vita kubwa ni kupiga vita dhidi ya umaskini; kwa vile Serikali ndiyo inayotoa ruzuku kwa Halmashauri ili kuwa na mtindo mmoja wa kuwasaidia hao Watendaji; je, ni kwa nini Serikali isikate fedha kutoka kwenye ruzuku za Halmashauri ili kuwapatia usafiri wa uhakika hao Watendaji ambao wanatembea kwa miguu katika maeneo ambayo ni makubwa sana, kwa ajili ya shughuli zetu za maendeleo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, zile ruzuku za Halmashauri ni ruzuku za maendeleo na zinapelekwa kwa ajili ya kufanya maendeleo katika Halmashauri husika, vijijini mpaka kwenye Kata. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, ninaziagiza Halmashauri kulingana na bajeti zao, waige mfano wa Wilaya ya Mufindi. Wilaya ya Mufindi, imewakopesha Watendaji wa Kata, kutoka kwenye *source* zao wenyewe, yaani kutokana na makusanyo yao wenyewe. Kwa hiyo, wamewanunulia Watendaji wa Kata pikipiki na wanawakata kidogo kidogo kutoka kwenye mishahara yao. Ndiyo maana, nimeziagiza Halmashauri kwamba, kutokana na unyeti wa suala hilo, Halmashauri ziwe zinapanga angalau kwa mwaka, kuwanunulia Watendaji wa Kata wachache na mwaka mwingine unaofuata wanawanunulie wachache, mwisho naona tatizo hili litakwisha.

Na. 111

**Muda wa Kusali**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania haina dini lakini Watanzania wana dini zao: Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ni busara kwa wafanyakazi kupangiwa kazi bila kuathiri muda wao mahsusi wa kuabudu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanya hivyo, napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaheshimika sana kutokana na amani, utulivu na mshikamano wa Kitaifa uliopo nchini; vitu ambavyo ni bidhaa adimu katika nchi nyingi duniani. Hata hivyo, amani na utulivu huo, vimejengeka katika misingi ya kuheshimu haki za Kikatiba za raia wetu, ikiwemo haki ya kuabudu, ambayo imeainishwa katika Ibara ya 19 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ingawa Tanzania kama nchi, haina dini. Ibara hiyo kifungu kidogo cha (3), ambacho kwa ridhaa yako naomba nikinukuu, kinasema hivi: "Hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii ya Katiba, itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na Sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa Kitaifa."

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Tanzania haina dini, lakini watu wake wana dini zao. Kwa kuzingatia ukweli huo, nchi yetu imeendelea kuheshimu uhuru wa kuabudu wa watu wetu, kwa kutoa fursa kwa watu wa dini na maadhehebu mbalimbali, wakiwemo wafanyakazi, kuendesha ibada zao kwa wakati muafaka, huku wakiendelea kuzingatia wajibu wao wa kazi katika kulijenga na kulileteа maendeleo Taifa letu. Utaratibu huu, umeendelea kuzingatiwa na kuheshimiwa na watu wetu bila manung'uniko kwa kipindi chote tangu tupate uhuru mwaka 1961. Aidha, haujaathiri muda mahsusi wa kuabudu wa watu wetu, dini zao na kila mtu yuko huru kufanya ibada katika muda muafaka, kama inavyoelekezwa na dini au madhehebu yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza wananchi wote wa Tanzania, kwa kuendelea kuzingatia utaratibu huo wa kuabudu bila kuathiri shughuli zao za kujiletea maendeleo na zile za kujenga Taifa. Wakati huo huo, natoa wito kwao, kuendeleza na kudumisha utaratibu huo, ambao umechangia sana kuwepo kwa amani nchini kwetu. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba, inawapangia kazi wafanyakazi bila kuathiri muda wao wa kuabudu; Serikali inafahamu kwamba, utaratibu wa sasa kwa wafanyakazi kama Maaskari Polisi na Trafiki, ambao hupangiwa kazi kukaa barabarani kwa ajili ya kusubiri misafara na mara nyingine hulazimika askari mmoja kukaa kutwa nzima, muda ambao kwa Muislam hulazimika kukosa vipindi vya swala zaidi ya vitatu; je, Serikali iko tayari kuurekebisha utaratibu huo ili askari hao wasinyimwe haki yao ya kuabudu?

La pili, pale ambapo askari kaondoka katika kituo chake cha kazi kwenda kuswali na kwa bahati mbaya au nzuri, mkuu wake wa kazi akapita na yeye hayupo na baada ya kurudi akachukuliwa hatua za kinidhamu, mfano kuhamishwa kituo cha kazi au nyingine. Je, hatua aliyochukuliwa ni sahihi kwa kuzingatia nchi ambayo ina Utawala Bora?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kwamba, hatujapokea lalamiko lolote, ambalo amelisemea Mheshimiwa Mbunge, iwapo tutalipata na kupitia kwake pia, tutashukuru na tutalishughulikia ipasavyo. Hata hivyo, napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge

na wananchi wote kwa ujumla kwamba, nchi yetu ina madhehebu mengi sana. Mkoa wa Mbeya wenyewe, naambiwa una madhehebu ya kikristo zaidi ya 300. Sisi tuna makabila mengi na koo zaidi ya 130 na kila mtu anaruhusiwa kuabudu anavyopenda, hata kama ni kutambika kwenye milima na kwenye mapango, maadam tu kuabudu huko, kusiingiliane na Katiba na shughuli za kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa Bunge halina dini lakini Waheshimiwa Wabunge wana dini zao; na kwa kuwa inajulikana wazi kwamba, siku ya Ijumaa kama leo ni siku ya Ibada Maalum kwa Waislam; kwa nini basi, Bunge linaruhusu kufanyika shughuli mbalimbali katika kipindi ambacho kinajulikana ni kipindi cha ibada kwa Waislam?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, naomba ubainishe tafadhali, kwa sababu huwa tunamaliza Shughuli za Bunge saa 7.00 mchana na swala ya adhuhuri siyo saa 7.00 mchana. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, huwa kuna *activity* kama semina katika Bunge, ambazo nadhani hufanywa kwa idhini ya Spika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwanza, umenisaidia kwamba, Shughuli za Bunge huwa zinaishia saa 7.00 mchana, wakati muda wa swala unaanza. Lakini kwa uzoefu wangu wa miaka zaidi ya 21 katika Bunge hili, sijawahi kusikia manung'uniko kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge yeyote kwamba, anakosa muda wa kuswali. Kwa hiyo, tungeomba hali hii iendelee, kama ni semina nadhani huwa mawasiliano yanafanyika kati ya waandalizi wa semina na Ofisi ya Mheshimiwa Spika, ili semina zifanyike baada au kabla ya wakati wa swala ya Ijumaa. *(Makofi)*

Na. 112

**Utekelezaji wa Programu ya MKURABITA**

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Handeni imepata bahati ya kuwa eneo la majaribio *(Pilot Study)* juu ya utekelezaji wa Programu ya MKURABITA hususan katika kupima maeneo ya wanavijiji ili wapatiwe hati za kumiliki maeneo ya ardhi; na kwa kuwa, mara mwanakijiji anapomilikishwa eneo hilo atakuwa amemilikishwa daima:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa, katika maeneo yenye ardhi ya kutosha ni vyema zikatungwa sheria za kuwaruhusu wanavijiji husika kugawana maeneo makubwa ili matumizi ya ardhi hiyo yafaidishe baba, mama, watoto, vijukuu, vilembwe na hata vitukuu vya kaya husika na sio baba na mama tu?

(b) Kama utaratibu wa MKURABITA ni kumilikisha wanavijiji maeneo madogo waliyonayo katika vijiji vyao ili kuwapa fursa ya kuwa na maeneo makubwa zaidi, yaani badala ya ekari nne wanaweza kumiliki ekari mia moja; je, Serikali haioni kuwa, hatua hiyo inapingana na dhana nzima ya kuwapunguzia wanavijiji umaskini?

(c) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili kiwango cha uelewa wa programu ya MKURABITA huko kwa wananchi vijijini. Imechukua au itachukua hatua gani kulingana na hali halisi?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

MKURABITA ni kifupi cha maneno, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania. Mpango huu ulianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2004. Madhumuni ya Mpango huu ni kuwawezesha wananchi wengi, wanaomiliki mali na biashara nje ya mfumo rasmi, kusajiliwa na kutambuliwa rasmi katika mfumo mpya wa kisheria ili waweze kupata fursa za kupata na kukuza mitaji katika soko rasmi la kisasa.

Mpango huu unatekelezwa kwa awamu nne. Awamu ya Kwanza ni tathmini ya Sekta isiyo Rasmi. Awamu hii ilianza tangu Oktoba, 2004 mpaka Desemba, 2005. Madhumini ya awamu hii ilikuwa ni kufanya tathmini ili kutambua ukubwa, thamani na kanuni za uendeshaji wa Sekta isiyo Rasmi. Awamu ya Pili ni Maandalizi ya Maboresho *(Reform Design)*. Awamu hii ilianza tangu mwezi Januari, 2006 na inaendelea hadi mwezi Oktoba, 2007. Madhumuni ya Awamu hii ni kuandaa sera na sheria zitakazowezesha kujenga mfumo mmoja wa umiliki mali na biashara Tanzania, kwa kuunganisha na kuboresha sheria na kanuni zinazotumiwa na wananchi katika Sekta isiyo Rasmi na zile zinazotumiwa na Sekta Rasmi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uzito wa kazi ya kuandaa maboresho, MKURABITA ilionelea ni vyema kuendesha mradi wa majaribio wa utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 katika Wilaya ya Handeni, katika vijiji saba vya Kweisasu, Sindeni, Mzeri, Bongi, Mbuyuni, Kwamkono na Nkale.

Awamu nyingine za MKURABITA, yaani Awamu ya Tatu na ya Nne ni utekelezaji wa Maboresho na Kuimarika kwa Mitaji na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza, ningependa kutoa ufafanuzi kuwa, MKURABITA haiwamilikishi wanavijiji maeneo ya ardhi, bali kwa kufuata Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999, maeneo ambayo tayari yanamilikiwa na wananchi katika vijiji hivyo yanarasimishwa, kwa maana nyingine kutambuliwa rasmi kwa kupimwa na kupewa hati miliki za kimila. Si MKURABITA wala Halmashauri ya Wilaya ya Handeni yenye mamlaka ya kuwamilikisha wananchi, maeneo madogo au makubwa, bali Halmashauri ya kijiji husika, imepewa dhamana ya kusimamia ugawaji wa ardhi ya vijiji vyao, kwa mujibu wa ibara ya 8 ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999.

(b) Mheshimiwa Spika, uzoefu wa MKURABITA katika vijiji hivyo saba, umeonesha ya kuwa wananchi wengi wanamiliki ardhi yenye ukubwa kati ya ekari 10 hadi 100, wachache wanamiliki ardhi ya zaidi ya ekari 100 hadi 200 na wachache

wanamiliki ardhi chini ya ekari 10. Kwa kuzingatia ukubwa huo wa ardhi na ukweli kuwa hati miliki za kimila hutolewa bila ukomo wa muda, wananchi wanaopata hati hizo watanufaika wao na familia zao, wajukuu na hata vilembwe.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa sasa ufahamu wa wananchi vijijini, juu ya MKURABITA, bado ni wa hali ya chini. Hii inatokana na ukweli kuwa, maandalizi ya maboresho yanayohitajika kuwezesha urasimishaji wa rasilimali na biashara kwa kasi zaidi, yanategemewa kukamilika ifikapo Oktoba, 2007. Hata hivyo, mpango mahsusi wa Habari, Elimu na Mawasiliano, juu ya Programu ya MKURABITA, utaanza kutekelezwa kuanzia Machi, 2007. Inategemewa kuwa, kuanzia hapo, ufahamu wa wananchi juu ya MKURABITA, utaongezeka kwa kasi. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa kuongeza ufahamu wa wananchi juu ya Programu ya MKURABITA, Serikali itaendelea kutoa taarifa na kuwasiliana na wadau katika kipindi hiki cha maandalizi ya maboresho *(Reform Design),* ili kukusanya maoni yao, yaweze kuwa sehemu ya maboresho yanayokusudiwa katika Programu ya MKURABITA.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Programu ya MKURABITA ni pamoja na kufufua mitaji mfu *(Dead Capital)* ya wanyonge huko Vijijini. Je, Serikali ina mkakati gani sambamba wa kuwahakikisha kuwa hili linafanikiwa ili madhumuni na malengo ya MKURABITA yaweze kufikiwa?

(b) Kwa kuwa dhana ya Uwezeshaji hasa ile ya kupunguza umaskini wa kipato, ambayo nayo vilevile inajumuisha MKURABITA ni moja ya Programu ya Uwekezaji nchini. Je, Serikali inaweza sasa kuunda Shirika au Taasisi inayojitegemea, kushughulikia masuala yote ya Uwezeshaji kama vile Programu ya Uwezeshaji, MKURABITA, mikopo midogo ili zoezi zima lifanywe kwa ufanisi zaidi kama inavyofanyika katika nchi nyingine za *SADC?*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu mkakati wa Serikali, Mpango ya MKURABITA bado upo katika majaribio na majaribio hayo kwa bahati nzuri, yameanzia katika Wilaya hiyo ya Handeni. Awamu ya Tatu na ya Nne bado hazijakamilika na inategemea sana matokeo ya majaribio hayo hasa katika Awamu ya Pili. Lakini pia inategemewa Serikali kukubali mapendekezo yatakayotolewa na hiyo Programu baada ya hayo majaribio. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira katika hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji na kuunda Shirika Maalum, pia katika hii Programu ya MKURABITA katika awamu zinazofuata inatarajiwa kwamba, kutakuwa na Taasisi zitakazohusishwa ama Taasisi nyingine zitaundwa ili kuratibu. Kwa hiyo, suala hili kwa sababu bado liko katika majaribio, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuvute subira. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea yapo masahihisho ya swali namba 124 la Wizara ya Fedha yaliyopo (a) na (b), imetolewa *addendum* hii. Kwa sababu baada ya swali kuhusika na Mifuko ya Hifadhi za Jamii, kukawa na masuala pia ya mbu,

ambayo hayahusiani na hilo, lakini ofisi imekwishatoa sahihisho. Niliona ni vizuri mlifahamu hilo.

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia kabla Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia hajasimama kujibu, napenda kutambua kwamba, Mheshimiwa Anna Killango Malecela, amekwenda kukaa mahali ambapo si pake pa kawaida. Ninachotaka kusema tu ni kwamba, ikiwa anatamani sasa kuhamia hapo moja kwa moja, alete ombi rasmi. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 113

**Udhibiti wa Silaha Nchini**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.N.Y. MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na ongezeko la ujambazi nchini; na kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na kwamba iliridhia *Protocol* ya *UN Plan of Action on Small Arms and Light Weapons:-*

(a) Je, mpaka sasa Serikali imefikia hatua gani katika suala zima la kuwa na *National Task Force* na wajumbe wake ni akinanani?

(b) Je, hadi sasa Serikali imefikia wapi katika mkakati mzima wa kushughulikia udhibiti wa silaha ndogo ndogo, za kati na za juu, juu ya uingizwaji wake hadi matumizi yake?

(c) Je, ni silaha ngapi haramu zimekamatwa na kuteketezwa hadi sasa na ni wahusika wangapi wamewekwa hatiani?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Taifa ya Kuratibu na Kudhibiti silaha ndogo ndogo na nyepesi, inajulikana kwa jina la *National Focal Point Committee for Small Arms and Light Weapons.* Jukumu la msingi la Kamati hii ni kusimamia na kuratibu masuala yote yahusuyo udhibiti wa silaha ndogo ndogo na nyepesi. Zipo pia Kamati za Mikoa na Wilaya, zenye jukumu la kutekeleza maamuzi ya Kamati ya Taifa. Kamati hizo za Mikoa na Wilaya, ndizo huitwa *Task Force*.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, aina za silaha zinazohusika na mpango huu ni silaha ndogo ndogo na nyepesi na sio silaha ndogo ndogo, za kati na za juu, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, naamini kuwa, swali la Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, lililenga kuulizia Kamati ya Kitaifa, yaani *National Focal Point Committee* na siyo *National Task Force,* ambayo haipo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tayari Serikali ilishaanzisha Kamati ya Taifa ya Kuratibu na kudhibiti silaha ndogo ndogo na nyepesi tangu Agosti, 2001.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wajumbe wa Kamati, kama ilivyo kwa Majeshi yote duniani, baadhi ya mambo huhifadhiwa na Majeshi husika na hayapaswi kutangazwa hadharani. Hivyo, hatutaweza kutaja majina ya Wajumbe wa Kamati hiyo. Endapo Mheshimiwa Mbunge bado ana nia ya kuwafahamu na iwapo Waheshimiwa Wabunge wengine wana nia hiyo hiyo, tutashukuru kushirikiana nao kwa kuwapatia majina hayo kwa utaratibu wenye siri zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa awali, upo utaratibu wa uingizwaji wa silaha nchini, ambao umewekwa bayana katika Sheria ya Kudhibiti Silaha na Risasi *(Arms and Ammunity Act No.2/1991* na *Armament Control Act No.1/1991)*, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa kanuni za sheria hizo na taratibu za kiutawala *(Administration Procedures*).

Hatua ya pili ya udhibiti ni kupitia katika Kamati za Ulinzi na Usalama, ngazi za Kijiji au Serikali za Mtaa, Wilaya na Mkoa, ambazo hupendekeza kama mwombaji aruhusiwe kumiliki silaha au kutomiliki. Aidha, hatua ya tatu ya udhibiti ni kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai *(DCI)*, ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kutoa kibali cha uingizwaji na umilikishwaji wa silaha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, Serikali pia imeanzisha Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kutokomeza Uzagaaji Holela wa Silaha Haramu *(National Action Plan)*, ambao utekelezaji wake ulianza rasmi Julai, 2001.

(c) Mheshimiwa Spika, toka kuanzishwa kwa Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kutokomeza Silaha Haramu, jumla ya silaha 9,157 za aina mbalimbali, zimekamatwa na kusalimishwa kati ya mwezi Julai, 2001 na Januari, 2007.

Aidha, silaha 8,539 tayari zimeteketezwa kwa moto na watuhumiwa 3,989 wamekamatwa kuhusiana na makosa ya kupatikana na silaha kinyume cha sheria na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza wananchi, kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa katika zoezi hili la udhibiti wa silaha haramu hapa nchini. Aidha, natoa wito kwa wananchi wote, kuwafichua wale wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 53 (d) inasema kwamba, Mbunge aliyekuwepo Bungeni wakati wa mjadala, hataruhusiwa kusoma gazeti, barua au kijarida chochote ila tu kama vinahusiana na shughuli ya mjadala unaoendelea wakati huo.

Wakati wa kipindi hiki cha maswali, nimemwona Mheshimiwa Halima J. Mdee, akisoma kijarida ambacho hakihusiani na mjadala wa hivi sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, inaonesha ulivyo makini katika kazi yako. Nitamwomba Mheshimiwa Halima J. Mdee, atulie asisome jarida, asubiri baada ya Shughuli za Bunge kwisha. Ahsante sana.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Sungusungu na Wanamgambo, ambao walisaidia sana kazi nzuri katika kuhakikisha kwamba, silaha ndogo ndogo zimepatikana kule na hatimaye Serikali imezifanyia kazi.

Sasa swali; je, Serikali imewaandaa vipi hao Wanamgambo na Sungusungu, ambao wanafanya kazi nzuri sana huko kwenye maeneo waliko, kupewa mafunzo ili waweze kuondokana na umaskini na kuwezesha kazi yao nzuri ya kufichua silaha kama hizi huko waliko?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sungusungu na Mgambo, wanafanyakazi nzuri huko kwenye maeneo yetu; je, Serikali inatambua kwamba wanawafanyia kazi nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kupitia utaratibu wa Polisi Jamii, tumeanza mpango wa kuwashirikisha Sungusungu na Wanamgambo, kusaidia mapambano ya uhalifu nchini. Hivi sasa Serikali kupitia Jeshi la Polisi, inaandaa utaratibu mzuri wa kisheria, utakaoweza kuwatambua hawa Sungusungu na Wanamgambo ili waendelee kushirikiana na Jeshi letu la Polisi katika kupambana na uhalifu.

Na. 114

**Shule za Jeshi**

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI (K.N.Y. MHE. MAGDALENA H. SAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jeshi limeanzisha shule kwa lengo la kuwasaidia Wanajeshi na familia zao katika kujiendeleza kielimu:-

(a) Je, JWTZ na JKT wana shule ngapi na ziko katika Mikoa gani na shule hizo zinatoza ada kiasi gani kwa lengo la kuwasaidia Wanajeshi?

(b) Je, Serikali inaelewa kuwa, baadhi ya Shule za Jeshi zina hali mbaya ya vifaa na majengo na kuna mpango gani wa kuzisaidia shule hizo?

(c) Kwa kuwa, shule hizo zinachukua pia watoto wa raia wa kawaida; je, Serikali Kuu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inatoa msaada gani kwa shule za jeshi?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, limeanzisha shule kwa lengo la kuwasaidia Wanajeshi na familia zao. Ongezeko la idadi ya watu katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, limefanya mahitaji ya shule pia yameonekana kuongezeka. Kwa mtazamo huo, Shule za Jeshi nazo zililazimika kupanua wigo na kuanza kuchukua watoto wa kiraia. Kwa kuwa Shule za Jeshi haziendeshwi kibiashara, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ilitoa maelekezo kwamba, ada kwa mwaka iwe Sh.150,000 kwa wanafunzi wa kutwa na Sh. 380,000 kwa wanafunzi wa bweni kwa mwaka. Hata hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imeruhusu kuongezwa ada baada ya Uongozi wa Shule na Kamati za Wazee, kukaa pamoja na kukubaliana kulingana na mahitaji ya shule.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi pamoja na JKT, wana jumla ya shule tisa za sekondari. Shule nne ziko katika Mkoa wa Dar es Salaam, nazo ni *Airwing, Navy* - Kigamboni na Jitegemee, zilizoko katika Wilaya ya Temeke na Makongo iliyopo katika Wilaya ya Kinondoni. Nyingine ni Ruhuwiko iliyoko Wilaya ya Songea Mkoa wa Ruvuma, Unyanyembe iliyoko Wilaya ya Tabora Mjini, Mkoa wa Tabora, Kizuka iliyoko Wilaya ya Morogoro Vijijini, Mkoa Morogoro, Kawawa iliyoko Wilaya ya Mufindi, Mkoa wa Iringa na Nyuki iliyoko katika Mkoa wa Mjini Magharibi kule, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupanda gharama za uendeshaji na kwa makubaliano ya Kamati ya Shule na wazee, Shule za Jeshi kwa hivi sasa zinatoza ada kati ya Sh. 200,000 hadi 300,000 kwa Shule za Kutwa na Sh. 500,000 hadi 580,000 kwa Shule za Bweni. Ada hiyo hutozwa kwa watoto wote, bila ya kujali kama anatoka katika familia ya Mwanajeshi au laa.

(b) Mheshimiwa Spika, hali ya majengo na vifaa katika shule saba kati ya tisa za Jeshi ni nzuri. Shule hizo hutenga fedha kila mwaka, kwa ajili ya ukarabati wa majengo na vifaa mbalimbali. Aidha, majengo ya shule mbili zilizosalia, pamoja na vifaa hayaridhishi. Shule hizo ni ile ya Nyuki - Zanzibar na *Navy* - Kigamboni. Hata hivyo, kwa kushirikiana na Kamati ya Shule na Wazee, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imekuwa ikichukua juhudi za mara kwa mara katika kurekebisha hali hiyo. Shule ya Navy, tayari imeshaanza kujenga majengo mapya na ile ya Nyuki, michoro ya majengo inaandaliwa na baadaye itatafutiwa fedha kwa ajili ya ujenzi. Lengo ni kuwa na shule bora kwa maana ya walimu, majengo na vifaa.

(c) Mheshimiwa Spika, misaada inayotolewa na Serikali imegawika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni lile la fedha taslimu *(cash)* na kundi la pili ni lile la bidhaa na vifaa mbalimbali *(in kind).* Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Ufundi, inatoa misaada kwa Shule za Jeshi katika maeneo yafuatayo: Semina za taaluma; mitihani ya wanafunzi; mitaala; ukaguzi wa shule; na walimu wa kushikizwa *(secondment).*

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia kwako, napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru sana Viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa misaada yao katika Shule za Jeshi. Nawaomba sana waendelee kuzisaidia Shule za Jeshi, kwa faida ya vijana na Taifa letu.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na najibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Hizi shule ambazo zinasimamiwa na Majeshi, zinapokea wanafunzi kutoka katika jamii ya Watanzania na Majeshi yetu kwa mujibu wa Katiba, ikiwa pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa ni maeneo ambayo hawatakiwi kujihusisha na siasa; sasa je, inakuwaje Shule ya Jitegemee ipambe Sherehe za Miaka 30 ya CCM?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Jeshi kama Jeshi, halihusiki na masuala yoyote ya kisiasa. Lakini Shule ya Jitegemee ni shule moja ambayo inayojitegemea, ina ukumbi na ukumbi huo unaweza kukodishwa na mtu yeyote, taasisi yoyote na chama chochote ili mradi utazingatia maelekezo tutakayoyatoa. Kwa maana hiyo, bado Jeshi la Wananchi, halijihusishi na masuala ya kisiasa na hatutajihusisha hata siku moja katika masuala ya kisiasa.

Na. 115

**Hitaji la Hakimu wa Wilaya – Bukombe**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali. Lakini naomba nitumie muda mfupi sana, kwa niaba ya wananchi wa Bukombe, nitoe shukrani zangu za dhati, kwa Mkutano Mkuu wa Chipukizi uliofanyika tarehe 28 Desemba, 2006, kwa kumchagua Lydia Richard Simon Mabenga, kuwa Mwenyekiti wa Chipukizi wa Taifa. Kwa hiyo, naomba salamu hizo zifikishwe kwa Wajumbe hao. Baada ya kusema hivyo, naomba kuuliza swali.

Kwa kuwa, uongozi wa Wilaya ya Bukombe na Baraza la Madiwani, wameamua kutenga moja ya majengo yake katika Wilaya ili litumike kwa shughuli za Mahakama; na kwa kuwa, wananchi wa Bukombe, wanapata shida sana kwenda Kahama kufuatilia kesi za Ki-Wilaya, umbali wa km 200 kwenda na kurudi:-

(a) Je, Serikali iko tayari kupeleka Hakimu wa Wilaya katika Wilaya hiyo?

(b) Kama jibu ni ndiyo; je, itakuwa lini ili wananchi wajiandae kumpokea na kero ya kufuata huduma hiyo kwa umbali huo itakuwa imetatuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sheria na Katiba, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye kipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula na uongozi mzima wa Wilaya ya Bukombe, kwa kutenga jengo hili litumike kama Mahakama pale Bukombe. Mheshimiwa Waziri, alipoitembelea sehemu ile, aliliona jengo hilo na alifurahishwa sana. Lakini nimweleze tu ni kweli kuwa, Mahakama ya Wilaya ya Bukombe, haina Hakimu Mkazi wa Wilaya. Hali hii inazikumba Wilaya nyingi nchini kutokana na uhaba wa Mahakimu wa kada hii. Hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa, Wilaya ya Bukombe inapata huduma za Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Tanzania, imemteua Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Kahama, kutembelea Wilaya ya Bukombe. Pia amepatiwa gari ili kumwezesha kuhudumia Wilaya zote mbili na pindi tutakapopata Mahakimu wa kutosha, Serikali basi tutahakikisha kwamba, atapelekwa Hakimu pale Bukombe.

**MHE. JAMES D. LEMBELI**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kesi zote za Mahakama ya Wilaya ya Bukombe hupelekwa Kahama na hivyo kusababisha msongamano mkubwa wa kesi za Bukombe na za Kahama pale Kahama Mjini; wakati huo huo kusababisha mlundikano mkubwa wa mahabusu na wafungwa katika Gereza la Kahama, lenye uwezo wa kubeba wafungwa na mahabusu 70, leo hii lina mahabusu na wafungwa wasiopungua 600; je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha kwamba, hali hii inaondoshwa pale Kahama na kuona kwamba mahabusu na wafungwa wanatendewa haki?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, tatizo la mlundikano katika Mahakama zetu, linatokana pamoja na mambo mengine na upungufu wa Mahakimu. Nimesema kwamba, Serikali sasa hivi inajitahidi kupata Mahakimu wa kutosha ili tuwapeleke katika kila Wilaya, waweze kujaribu kupunguza mlundikano huu. Ni jana tu magazeti yetu ya nchi, yalitangaza nafasi 85 za Mahakimu wa Mkoa. Kwa hiyo, tunategemea tukiwapata hao, tutapeleka kule Bukombe na Kahama ikiwezekana ili tuweze kupunguza mlundikano ambao uko pale.

Na. 116

**Upatikanaji kwa Vyeti vya Kuzaliwa**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kuwa, upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa umekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Magu, ambao hulazimika kutumia gharama kubwa kuvifuata Makao Makuu ya Wilaya: Je, kwa nini Serikali isisogeze huduma hii kwenye Serikali za Vijiji, Zahanati na Vituo vya Afya?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nne wa Bunge lako Tukufu, wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge Viti Maalum, nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa, kupitia Sheria Na. 19 ya 2005, huduma za kuandikisha vizazi, zimesogezwa karibu zaidi na wananchi, tofauti na ilivyokuwa hapo awali, ambapo usajili huo ulifanyika katika Ofisi ya Msajili wa Vizazi na Vifo katika Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa vyeti vya kuzaliwa kwa raia wake. Vyeti hivi ni muhimu kwa usalama wa nchi yetu, uthibitisho wa uraia na maslahi ya Taifa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa vyeti hivyo vya kuzaliwa, utoaji wake ni lazima udhibitiwe. Hivyo basi, vyeti hivyo hutolewa tu na wasajili wa vizazi kwa mamlaka waliyopewa kisheria.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa vyeti vya kuzaliwa vinapatikana kwa wakati muafaka na kwa ubora unaokubalika, Serikali imechukua hatua za makusudi za kuibadilisha iliyokuwa Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali, kuwa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini. Wakala huyu kupitia mpango mkakati wake, ameazimia kusogeza huduma za usajili kwa wananchi kwa kutumia magari na pikipiki *(Mobile Services).* Aidha, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, anafanya mapitio ya Sheria na taratibu zinazohusiana na shughuli zake, hususan za usajili wa vizazi, kwa lengo la kupunguza kero za wananchi na kuboresha huduma.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa jimbo langu la Magu, wamenituma nieleze kero hii kwamba, wanapata kero kubwa sana kufuatana na kusajili uzazi pamoja na vifo. Mheshimiwa Waziri, katika jibu lake amesema kwamba, huduma hii ya kuandikisha vizazi imesogezwa karibu zaidi na wananchi.

Ataweza kueleza zimesogezwa vipi karibu na wananchi, kwa maana kusogea Wilayani ndiyo karibu zaidi na wananchi; je, asingeona kwamba kuna haja ya kusogeza zaidi kwenye vituo vya afya angalau zitolewe Kitarafa badala ya kutolewa Kiwilaya na ikiwezekana zitolewe Kikata?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa vyeti hivyo hulipiwa shilingi 10,000 na wananchi walio wengi ni maskini; je, Mheshimiwa Waziri, haoni haja ya kupunguza bei hiyo ili angalau iwe shilingi 5,000, wananchi waweze kuimudu?

**SPIKA:** Nadhani Mheshimiwa Mbunge, anaposema bei ana maana ada.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilisema kwamba, huduma hizi zimesogezwa. Zimesogezwa vipi?

Huduma hizi sasa hivi mtoto akizaliwa au mtu akifa katika kijiji, basi taarifa zake huandikishwa pale kisha zinapelekwa Wilayani kuchukuliwa cheti tu.

Kwa hiyo, pale pale kwenye zahanati au kijijini kwa Afisa Mtendaji au kwenye Kata, taarifa zinaandikishwa, zinapelekwa moja kwa moja Wilayani kuchukuliwa cheti. Hatuwezi tukapeleka vyeti vikagawiwa pale kijijini au kwenye zahanati, tutashindwa kudhibiti kutoa vyeti hivi ambavyo ni muhimu sana kwa ujumla katika Taifa letu.

Kuhusu suala la ada shilingi 10,000, kwa kweli vyeti hivi ni lazima vitengenezwe katika hali ambayo haviwezi kuwa-*forged* kwa urahisi, haviwezi kupatikana ovyo ovyo. Kwa hiyo, ubora wake ni wa hali ya juu na gharama yake si ndogo.

Kwa hiyo, tunavyoweka hizi shilingi 10,000, kwa kweli ni gharama za utengenezaji tu wala sio gharama ambazo zina faida juu yake. Kwa hiyo, naomba wananchi wa Magu, wajitahidi walime pamba zaidi, waweze kumudu bei ya vyeti hivi. *(Makofi)*

Na. 117

**Posho za Wazee wa Baraza**

**MHE. LUCY T. MAYENGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imedhamiria kupambana na rushwa kwa nguvu zote; na kwa kuwa, bado posho za Wazee wa Baraza ni ndogo sana na hazilipwi kwa wakati:-

(a) Je, ni lini Wazee wa Baraza wataongezewa posho zao na ni lini tabia ya kuwakopa Wazee wa Baraza itakoma?

(b) Je, kitendo cha kushindwa kuwalipa kwa wakati wazee hao, Serikali haioni kuwa inajenga kishawishi cha rushwa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sheria na Katiba, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imedhamiria kupambana na rushwa kwa nguvu zote. Naomba ieleweke kuwa, ukubwa wa mishahara au posho pekee, sio kigezo cha kumzuia mla rushwa mzoefu kuacha kula rushwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, si sera ya Serikali kuwakopa Wazee wa Baraza. Serikali inathamini mchango wa Wazee wa Baraza hivyo, imekuwa ikihakikisha kuwa, Wazee hao wa Baraza, wanalipwa posho zao kwa wakati kwa kupeleka fedha za posho za Wazee wa Baraza kwenye Mahakama za Wilaya, mara tunapozipata kutoka Hazina. Posho za Wazee wa Baraza hulipwa pale kesi wanazosikiliza, zinapomalizika na maamuzi kutolewa, kwa kuzingatia siku walizohudhuria usikilizwaji wa kesi hizo.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuchukua fursa hii, kuwaonya baadhi ya watumishi wa Mahakama, ambao si waaminifu, kuacha mara moja, tabia ya kukopa fedha za kuwalipa wazee wa Mahakama. Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa, dhidi ya watumishi wenye tabia hiyo. Kadhalika napenda kutoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge kuwa, kama anaifahamu Mahakama ambayo wazee wake wa Baraza hawajalipwa kwa muda mrefu, atupatie taarifa ya madai hayo ili utaratibu wa malipo ya wazee hao ufanyike mara moja.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Baada ya majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri; je, Serikali itakuwa sasa tayari kuweza kuhakikisha kwamba, usumbufu huu wa Wazee wa Baraza, ambao wamekuwa wakiupata katika maeneo mengi hasa vijijini kama kule kwetu Shinyanga, unakwisha kwa maana ya kwamba kiwango cha 1,500 cha kesi ambacho mzee wa Baraza analipwa mpaka kesi iishe; kwanza kabisa hakitoshi kwa sababu Mahakama nyingi zimekuwa zikitoa Wazee wa Baraza kutoka maeneo mengine na imekuwa ikichukua muda mrefu, hali ambayo inasababisha kuweka mazingira ambayo yanaweza yakachochea suala la rushwa?

Swali la pili; je, Serikali iko tayari sasa kuweza kuhakikisha kwamba, inabadilisha mfumo mzima wa Wazee wa Baraza katika maeneo ya mijini, ambapo wamekuwa ni wazee wale wale kwa muda mrefu, sasa hivi waweze kubadilishwa kulingana na hali halisi ya maisha ilivyo sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Vijana, kwa kushughulikia vilivyo matatizo ya wazee, hasa Wazee wa Baraza na hasa wazee wa Shinyanga pia.

Kiasi wanacholipwa wazee hawa kinaonekana ni kidogo, lakini wazee hawa ni wazee walioko kwenye ile *locality* si kwamba, wana gharama za usafiri au namna gani. Wazee wa pale pale tu na kwa kawaida, wanaitwa wazee wa pale ili kumshauri Hakimu kuhusu mila na taratibu za pale pale. Kwa hiyo, gharama zao za kufika pale Barazani kama ambavyo wao wanapaita, kwa kweli si kubwa sana, ingawa nakubali kiwango hiki pengine Serikali itakaa sasa ikitazame upya. Kuhusu suala la kuwabadili hawa wazee wabadilishwe hasa mjini ili tupate sijui wazee wa kisasa na hili niseme kwamba, nia ya hizi Mahakama za Mwanzo kuweka Wazee wa Baraza ni hasa kuwashauri katika masuala ya *customary law,* kwa *customs* ambazo ziko pale. Kwa hiyo, wazee hawa wanafaa wawe wale wale maana, yake ndiyo wanaozijua na ndio wa pale pale.

Na. 118

**Ukosefu wa Wataalam wa Ugani**

**MHE. MUHAMMED AMOUR CHOMBOH** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, kuna mikakati ya kukuza na kuendeleza kilimo cha kisasa kwa nia ya kuongeza mavuno mengi na mazuri; na kwa kuwa, bila ya kuwa na wataalamu wa ugani wa kuwaelimisha wakulima njia nzuri za kilimo cha kisasa, mavuno mazuri hayatapatikana mashambani; na ili kuondoa tatizo la maafisa ugani kutokubali kwenda mashambani kwa wakulima:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, ni vizuri sasa kuwatafuta na kuwafundisha vijana wanaomaliza Sekondari kuwa maafisa ugani kwa kila Wilaya husika?

(b) Kwa kufanya hivyo; je, Serikali haioni kuwa, itatoa ajira kwa vijana hao na wakati huo huo kuwasaidia wakulima kupata maafisa ugani ambao ni wenyeji wa Wilaya husika na hivyo kuondoa tatizo la wataalam hao kutowafikia wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, wataalam wa ugani ni muhimu katika kuwaelimisha wakulima njia bora za kilimo cha kisasa na hivyo kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za ugani nchini, Wizara yangu imeandaa andiko, ambalo litatoa mapendekezo ya kuimarisha huduma hizo. Mapendekezo hayo ni pamoja na kugharamia ajira mpya za wataalam wa ugani; kugharamia mafunzo kwa vijana katika Vyuo vya Kilimo, ambao hatimaye wataajiriwa kama maafisa ugani; na kutoa vitendea kazi kwa Maafisa hao ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za kuishi. Aidha, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kutoa wito kwa Halmashauri za Wilaya, kutenga kiasi cha fedha zinazotolewa chini ya Mpango wa *ASDP*, kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi *(Capacity Building)* wa wataalam wa kilimo waliopo na kuchangia upatikanaji wa vitendea kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya Mwaka 2005, imeeleza bayana, lengo la Serikali ya Awamu ya Nne kuwa na ajira mpya zaidi ya milioni moja katika kipindi hiki cha miaka mitano. Napenda kusisitiza kuwa, mapendekezo ya ajira mpya za maafisa ugani zaidi ya 12,000 yanayoandaliwa, yanalenga kutekeleza Ilani hiyo na pia kuondoa tatizo la upungufu wa maafisa ugani vijijini. Aidha, haitakuwa busara kulenga kupata maafisa ugani ambao ni wenyeji wa Wilaya husika tu kwa lengo la kuwafikia wakulima kwa urahisi vijiji wanapoishi. Hivyo, maafisa ugani wanaohitimu, wanaweza kupelekwa sehemu yoyote kutoa huduma kwa kuwa, kila Mtanzania anayo haki ya kufanya kazi mahali popote ndani ya mipaka ya nchi yetu.

. **MHE. MUHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Nataka kujua Wizara ya Kilimo ina mikakati gani ya dharura ya kuwashawishi vijana au maafisa ugani, kwenda mashambani sasa hivi hasa ukizingatia kwamba, mvua zimenyesha vizuri na tunategemea kwamba mazao yatakuwa ni mazuri zaidi? Je, kuna mikakati yoyote ya dharura sasa hivi, kuweza kuwahamasisha vijana hao kufika mashambani kwa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, wataalamu wa ugani walioko mawilayani, tunawaasa waendelee kufanya kazi yao kwa sababu wanatakiwa kufanya hiyo kazi. Lakini kwa sasa hivi katika mpango ambao tunausema wa kuimarisha huduma za ugani

nchini ni pamoja na kuajiri vijana ama wataalamu 2,500 wanaotokana na wale waliomaliza vyuo vya kilimo, ambao wako nyumbani ama wako mitaani hawana kazi.

Vijana 2,500 kutoka Vyuo vya Kilimo vile tisa, pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine. Lakini pia tuna mpango kama nilivyosema kwamba, tunaandaa mpango, unaohusisha kusomesha vijana 8,500 ambao utagharimu shilingi bilioni 6.4 na pia tunatakiwa tupeleke vitendea kazi. Kila wilaya inatakiwa iwe na gari na hivyo tunafikiria kuwa na bajeti hiyo ya magari 121, pikipiki 6,500 na halafu baiskeli 9,000 kwa ajili ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna mpango wa kuwajengea nyumba na katika mpango wetu tunakisia kuwa na nyumba 2,700 na kuwapatia vile vile kama kamera, vinasa sauti ambavyo vitaweza kuwasaidia pamoja na *extension kit* ambazo zitawasaidia katika huduma hii ya ugani. Lakini vile vile tunatakiwa tuimarishe vile vyuo vyetu vya kilimo ambavyo vipo na kujenga *Ward Resources Centres* yaani vituo vya Kata kwa ajili ya huduma ya kilimo katika ngazi za Kata na vile vile tuongeze mabweni katika zile *Training Centre* kwenye maeneo yale ambayo wakulima wanafundishiwa kilimo kusudi waweze kupata nafasi kwa wingi zaidi kupata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za ugani, vile vile tunategemea kwamba tutaajiri wakufunzi 258 kusudi waweze kutoa mafunzo haya ya wataalam ya ugani 8,500 kwa awamu nne. Awamu ya kwanza itachukua asilimia 40, awamu ya pili asilimia 40, awamu wa tatu na ya nne itachukua asilimia kumi kumi. *(Makofi)*

Na. 119

**Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuanzia mwaka 2002/2003 Serikali imeendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji mashambani katika skimu za Muhwazi, Ruhwiti na Katengera kwa mafanikio makubwa; na kwa kuwa, wananchi wamehamasika na kilimo hicho lakini uwezo wao ni mdogo na zana wanazotumia ni duni:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia mafanikio yaliyokwisha patikana ili kuendeleza mabonde mengine ya Ruguzye, Mugondogondo, Kilemba, Mugoboka, Mwiruzi na Muyorozi;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kueneza matrekta katika Wilaya ya Kibondo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE.CHRISTOPHER K. CHIZA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza wakulima wa skimu za umwagiliaji za Muhwazi, Ruhwiti na Katengera kwa jinsi walivyoitikia wito wa Serikali na kutekeleza miradi yao ya umwagiliaji kwa mafanikio makubwa na kuongeza tija katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabonde yote aliyoyataja Mheshimwa Mbunge yamekwishaainishwa katika Mpango kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji wa mwaka 2002. Linalotakiwa kufanywa sasa ni Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo kuingiza mabonde hayo katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya kwa ajili ya utekelezaji. Kwa utaratibu huu, tayari mabonde ya Mugondogondo na Mwiruzi yameingizwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2006/2007 na ujenzi wa banio kwenye Mto Mwiruzi na mfereji wenye urefu wa kilometa mbili umechimbwa na kazi inaendelea. Bonde la Mto Ruguzye litaanza kufanyiwa kazi katika mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Aidha, napenda kutoa tahadhari kwa uongozi wa Wilaya ya Kibondo na Wilaya nyingine zilizo mipakani kwamba uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji kwenye mito ambayo vyanzo vyake viko katika nchi jirani inahitaji maelewano kati ya pande mbili ili kuepuka athari za kukosa maji wakati nchi hizo jirani zikizidisha matumizi ya maji kwa upande wao. *(Makofi)*

Mradi wa Mwiruzi ni mojawapo ambao chanzo cha mto wake kiko katika nchi ya Burundi. Tarehe 16/1/2007 Ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Kibondo ulifanya mazungumzo na Ujumbe wa Burundi ulioongozwa na *Governor* wa Jimbo la Chankuzo kuhusu ujenzi wa mradi wa umwagiliaji wa Mwiruzi. Katika mkutano huo uliofanyika kwenye eneo la ujenzi wa mradi wa Mwiruzi viongozi hao walikubaliana kuendeleza mazungumzo ya ujirani mwema na matumizi ya maji ya mto Mwiruzi kwa faida ya pande zote mbili. Maelewano kama haya hayana budi kutangulia wakati wa kuanzisha miradi ya namna hiyo kuepeka athari zinazoweza kutoka ukizingatia kwamba miradi yetu ndiyo iko chini yaani *down stream* kufuatia mtiririko wa maji ya mito.

(b) Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma ni mmojawapo kati ya Mkoa wenye matrekta machache sana ambapo Mkoa mzima una matrekta mawili tu yanayofanya kazi. Aidha, Wilaya ya Kibondo haina trekta zima hata moja. Suala la matumizi ya matrekta katika Wilaya ya Kibondo linahitaji kwanza uongozi wa Mkoa wa Kigoma kuwahamasisha wakulima, wafanyakazi na wafanyabiashara ili waone umuhimu wa matumizi ya trekta. Wakulima hawana budi kuhamasishwa kuandaa mashamba ikiwa ni pamoja na kung'oa visiki. Kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kwamba kati ya mwaka 1986 na 1993, Serikali kupitia Benki Kuu na *CRDB* iliandaa mpango wa kuwakopesha matrekta wakulima. Matrekta 80 yalipelekwa mkoani Kigoma ambapo walitakiwa kulipa asilimia kumi ya bei ya trekta. Wakulima kwa bahati mbaya walishindwa kulipa na *CRDB* ililazimika kuyahamisha matrekta yote kupeleka Mikoa mingine.

Napenda kutoa wito kwa uongozi wa Mkoa wa Kigoma kuwahamasisha upya wakulima na wafanyabiashara ili watumie fursa ya mikopo kutoka katika Mfuko wa Pembejeo na vyanzo vingine ili waweze kuwa na matrekta yao na wengine waanzishe vituo vya kukodisha matrekta. Aidha, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo kufufua mazungumzo yaliyokwisha anza na Mfuko wa Pembejeo, kutafuta uwezekano

wa Halmashauri hiyo kudhamini waombaji wanaotaka kununua matrekta. Naamini ushauri huo pia utazinufaisha Halmashauri za Wilaya nyingine. *(Makofi)*

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Baada maelezo mazuri kutoka kwa Naibu Waziri ninaomba kuuliza maswali mawili madogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, kwa kuwa tarehe 24/10/2004, aliyekuwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja alifanya ziara Wilayani Kibondo na akawakuta wananchi wa Bonde la Mgondogondo wakifanya kazi za kilimo hicho; na kwa kuwa baada ya kuona ama kuwaonea huruma wananchi hao walivyokuwa wakifanya kazi aliahidi kwamba Serikali ingeweza kuwasaidia shilingi milioni 150 kwa ajili ya kuwawezesha kufanikisha kilimo hicho, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo hata kama awamu imeshapita? *(Makofi)*

Mheshimiw Spika, pili, Mkoa wa Kigoma unajitahidi sana kuhakikisha kwamba chakula kinachozalishwa pale kinatosheleza wananchi wake ikiwa ni pamoja kusaidia mikoa ya jirani. Lakini kwa bahati mbaya mazao yanayolimwa katika Mkoa huo yanalimwa kuwa kutumia jembe la mkono, je, Serikali haioni kwamba Serikali kwa makusudi mazima inaweza ikaandaa mkakati wa kuweza kuwasaidia wanannchi hawa wanaojitahidi na kulisha Mikoa na nchi ya jirani na kuwapatia matrekta ili kuendeleza kilimo ambacho kitawawezesha kulisha mikoa na nchi nyingine zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE.CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi wa aliyekuwa Waziri wa Kilimo ya shilingi milioni 150, kwanza napenda kusahihisha kidogo kwamba mimi mwenyewe nilikuwepo katika ziara hiyo nikiwa Mkurugenzi katika Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Charles Keenja hakuahidi kutoa shilingi milioni 150 isipokuwa alimwagiza Mhandisi wa Umwagiliaji wa Kanda ile kuandaa andiko ili liweze kupelekwa *Tanzania - Japan Food Aid Counterpart Fund* ambao katika kipindi hicho ulikuwa na *ceiling* ya shilingi milioni 150. Kwa hivyo. Mheshimiwa Charles Keenja alikuwa amemuagiza mtaalam yule kuandaa andiko. Nafurahi kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba andiko limekwishapelekwa katika mfuko huo na mimi nitafuatilia kuhakikisha kwamba pesa hizo zinapatikana. *(Makofi)*

Kuhusu matrekta kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi iko haja ya Mkoa kujipanga upya. Kwanza kuwahamasisha wakulima kung'oa visiki katika mashamba yale ya bega kwa bega Mkoani Kigoma. Lakini pia kama Wizara nataka nimuahidi kwamba tutatuma wataalam wa zana za kilimo na wale wa mfuko wa pembejeo ili kusaidia kuhamasisha wananchi na kuwaelekeza namna ya kujaza fomu ili hatimaye waweze kupata mikopo hii kwa ajili ya kuanzisha vituo na wengine matrekta yao binafsi.

Kwa hiyo, leo nadhani kila Mheshimiwa Mbunge amepata zile fomu mbili za kuomba mikopo ya matrekta na pembejeo na kama hazitaeleweka basi tunaomba muwafate wataalam wa kilimo Wilayani na hata Wizarani tuwasaidie. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana, nathibitisha hata Mheshimiwa Spika amezipata hizo fomu. Tunahamia swali linalofuata bado Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Alyoce Kimaro, Mbunge wa Vunjo.

Kabla hujauliza Mheshimiwa Kimaro ninataka kusema kwamba kwa namna ulivyobadili wajihi, ungependeza zaidi kama ungevaa vazi kama la Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi. Sasa unaweza kuuliza swali lako. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa ushauri wako, sasa nitakutana na Waziri wa Ulinzi tupeane ushauri zaidi. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 120

**Mabwana kwa Ajili ya Umwagiliaji**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufunga mito ya Whona na Muwe ili kuweza kupata mabwawa ambayo yatatumika kwa umwagiliaji katika Kata ya Makuyuni, Kilema Kusini, Kirua Kusini, Kahe Mashariki na Magharibi? *(Makofi)*

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza mfereji wa Kimwangamao uliopo Kahe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE.CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo ya jumla ifuatavyo:-

Ripoti za Mapngo kabambe wa maji wa Mkoa wa Kilimanjaro *(Kilimanjaro Water Master Plan), 1977* na mpango kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji *(National Irrigation Master Plan), 2002* zinaonyesha kwamba matumizi ya sasa ya maji ni makubwa hasa katika miezi ya Januari na Februari na uwezekano wa kuwa na upungufu mkubwa wa maji katika miezi hii miwili ni mkubwa sana. Aidha, kasi ya kuongezeka kwa watu na mahitaji yao ya maisha bora kunaongeza mahitaji ya maji. Katika hali hii, mikakati inayopendekezwa kuondoa tatizo la uhaba wa maji ni kuboresha matumizi ya maji yaliyopo na kutafuta vyanzo vingine vya maji ikiwa ni pamoja na kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji na kuchimba visiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Kimaro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka 2004, Wahandisi wa umwagiliaji wa Wizara yangu walifanya uchunguzi wa awali wa sehemu zinazofaa kwa ujenzi wa mabwawa *(Dam sites)* kwenye Mto Muwe, Mto Whona na Mto Mbwambo. Uchunguzi huo unaonyesha kwamba *catchments areas* zilizopo ni ndogo kiasi kwamba mabwawa yatakayojengwa hayataweza kuhifadhi maji ya kutosha kwa kilimo cha umwagiliaji. Kwa mfano, bwana litakalopatikana kwa kuziba kwenye makutano ya Mto Whona na Mto Unna linakadiriwa

kuwa na ujazo wa 500,000$m^3$ za maji ambayo hayatoshi kwa kilimo cha umwagiliaji unaotarajiwa.

Aidha, kutokanana maporomoko *(steep slopes)* katika mito hiyo, njia ya kuziba ni ya kujenga kwa zege ambayo ni gharama kubwa ukilinganisha na kiasi cha maji kitakachohifadhiwa. Wizara yangu inatarajia kukamilisha uchunguzi wa kina wa ujenzi wa mabwawa yaliyopendekezwa kwa kuangalia masuala mengine yanayohusu aina ya tuta litakalojengwa *(Earth Embankment Dam or Concrete Gravity Dam),* athari za mazingira zinazoweza kutokana na kuwepo kwa mabwawa, mali za watu zinazoweza kuhitaji fidia na kuandaa gharama halisi za ujenzi. Kabla ya kufikia uamuzi wa kujenga au kuacha. Kwa upande mwingine, taarifa za kujiolojia zilizopo zikichanganywa na kuwepo kwa visima virefu vya Miwaleni na Chemchem ya Miwaleni, ni ushahidi wa kutosha kwamba eneo la Kahe pia hunufaika na maji ya ardhini.

(b) Mheshimiwa Spika, mfereji wa Kimwangamao unaojumuisha vijiji vya Kisangesangeni, Mwangaria, Ngasini, Mawala na Oria unapata maji yake kutoka katika chemchem ya Miwaleni na unayo hati ya kumiliki maji *(water right)* ya kiasi *cha 1.0*$m^3$*/sec.* Kinachotakiwa kufanywa ni kukarabati na kuboresha mfereji huo ambao una urefu wa kilometa 7.5 hasa kwa kupunguza upotevu wa maji kwa kusakafia sehemu korofi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali imetoa shilingi milioni 14 kama ruzuku ya maendeleo kutoka katika *Local Government Capital Development Grant* kwa ajili ya kuboresha mfereji wa Kimwangamao. Fedha hizi hazitoshi, zinahitaji fedha za ziada ili kufanya kazi nzuri. Nimewaagiza wataalam wa Ofisi ya Kanda ya umwagiliaji ya Kilimanjaro kuandaa gharama za ukarabati wa mfereji huo kwa ajili ya kuombewa fedha za utekelezaji chini ya *ASDP*. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema sehemu za Kahe na Miwaleni wanaweza kufaidika na maji kutoka ardhini kwa kuchimba visima virefu. Swali je, Serikali kwa kupitia Wizara yake ina mpango gani wa kuchimba hivyo visima?

La pili, kwa kuwa Serikali kwa kupitia majibu ya Naibu Waziri amekubali kwamba mfereji wa Kimangamahu, pesa zilizotolewa milioni 14 hazitoshi kabisa, ameagiza wataalam wafanye upembuzi yakinifu ili tuweze kuomba fedha kutoka *ASDP.* Je, Serikali ipo tayari kutoa fedha hizo katika mwaka huo wa 2007/2008 ili mfereji huo utengenezwe kwa ukamilifu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE.CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu visima virefu kule Kahe, kama tulivyokwishaeleza mara nyingi kwamba miradi inatakiwa iandaliwe, iletwe iwekwe katika programu ya *ASDP* kupitia *DADPS* basi hata hivyo visima vya Kahe nivyo ni sehemu ya mradi.

Kwa hiyo, wataalam wa Wizara ya yangu wanapokwenda kule pamoja na wale wa Wizara ya Maji tunawatumia pia, watakusaidia kuangalia ni visima vipi vinaweza

kuchimbwa na yataandaliwa maandiko katika *DADPS* na yakishafikishwa tutayatizama kwa pamoja miradi mingine chini ya *ASDP. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa fedha za mradi huu kwa mwaka 2007/2008, ninachoweza kumwambia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba mwaka 2007/2008 bado bajeti yake haijazungumzwa ni mapema mno kuzungumzia Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, lakini kinachotakiwa sasa ni kuhakikisha kwamba utaratibu unaandaliwa mapema, miradi hii ifanyiwe makadirio ili itakapoibuliwa kama itakuwa inakidhi mahitaji ni *serable project.* Namhakikishia kabisa kwamba tutaingiza katika mpango wa mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Na. 121

**Mikopo ya Pembejeo kwa Wakulima**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Makampuni ya Tumbaku yamekuwa yakichukua asilimia mia moja ya madeni yao ya pembejeo kutoka kwa wakulima bila kujali athari wanazopata wakulima kama vile mafuriko, mvua za mawe, ukame na kadhalika hali inayosababisha vyama vya msingi na wakulima kuwa na madeni:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kuhakikisha kuwa yanapojitokeza majanga kama hayo hasara hiyo inagawanywa kwa wakulima na makampuni ya Tumbaku?

(b) Je, Serikali haioni kuwa utaratibu wa kuwapanga wakulima kumi ili wakopeshwe inaongeza hatua ya kuongeza madeni na kuwasababishia wakulima waaminifu kukosa kipato kwa kulipa madeni ya wale wasio waaminifu, kwa nini utaratibu wa zamani wa kila mkulima kujidhaimini na kulipa deni lake mwenyewe usirejeshwe?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kunapotokea majanga ya mafuriko, mvua za mawe, ukame, na kadhalika kwenye zao la tumbaku ni kweli kwamba Serikali haijaingilia kati kugawanya hasara inayotokana na majanga kati ya wakulima na Makampuni ya Tumbaku. Hii imetokana na mfumo unaotumika katika uzalishaji wa zao la tumbaku. Kilimo cha tumbaku kinakuwa cha mkataba kati ya Vyama vya Msingi kwa niaba ya wakulima na Kampuni za Tumbaku.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Wizara yangu itapeleka mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge kwenye vikao vya wadau wa tumbaku ili tupate muafaka juu ya utaratibu unaoweza kutumika endapo wakulima watakumbwa na majanga mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli upo utaratibu wa kuwapanga wakulima kwenye vikundi vya wakulima kumi kwa ajili ya kukopeshwa. Utaratibu huu ambao unatokana na makubaliano ya wanachama wenyewe kupitia vyama vya msingi, unasimamia na kudhibiti wakulima wachache ambao sio waaminifu. Kwa mfano, katika maeneo ya Kahama, Bukombe, Mpanda na Chunya ambako vikundi hivyo vya kusimamia viliundwa na kuwajibika ipasavyo, tatizo la kutolipa madeni na fedha za wakulima limepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iko katika mchakato wa kutafuta mfumo mbadala ambao utaboresha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima wa tumbaku na pia uuzaji wa zao la tumbaku. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa utaratibu ninaopendekeza wa wakulima mmoja mmoja ulikuwepo zamani. Mkulima mmoja mmoja alikuwa anajidhamini na unaweza ukaboreshwa vizuri sana kwa kumruhusu kila mkulima wakati mitumba yake inanunuliwa naye awepo ndani sokoni, je, Serikali iko tayari kutoa maelekezo kama iliyoyatoa wakati anajibu swali langu kwenye sehemu (a) ili utaratibu wa sasa wa kumweka nje mkulima wakati tumbaku yake inanunuliwa ndani uweze kufanyiwa marekebisho? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa lengo la Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwenye sekta hii ndogo ya tumbaku ni kuhakikisha kwamba tunafikia tani 100,000 kufikia mwaka 2010, je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuruhusu muungano wa makampuni ya tumbaku unaoitwa *ATTT* ni sababu kubwa sana ambayo inaendelea kuhakikisha kwamba wakulima wetu kupitia muungano huu wanaendelea kukandamizwa na kunyonywa katika mazingira ambayo Serikali ingeweza ikatoa maelekezo haya makampuni yakaendelea kufanya kazi yakiwa kampuni peke yake kuliko kutumia muungano huu ambao unaendelea kuwanyonya wakuliwa wetu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu kama nilivyosema kwamba kilimo cha tumbaku na kuuza tumbaku au kupata mbejeo kunatokana na mikataba kati ya wakulima na yale makampuni nadhani kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge na yeye ni *member* wa Bodi ya Tumbaku tutashirikikiana naye pamoja na Wizara pamoja na wadau wengine wa tumbaku kusudi tuweze kubadilisha utaratibu huo kusudi wakulima nao waweze kuruhusiwa kuona tumbaku yao inavyouzwa na waweze kuthibitisha ubora na *grade* za tumbaku ambayo wanaiuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kama nilivyoseme mwanzoni kuhusiana na utaratibu mzima wa tumbaku na kwamba malengo yetu ni kufikia tani laki moja ifikapo mwaka 2010 na katika kumpa haki yule mkulima aweze kupata bei nzuri bila kukandamizwa na makapuni ya *ATTT,* basi ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakaa pamoja na wadau wa zao hili na wanunuzi na kama tulivyosema sisi tunachotaka sasa hivi ni kuimarisha ushirika kusudi ushirika huu uweze kutoa matatizo hayo yanayohusiana na kupewa mikopo na hiyo *ATTT*. Kwa hiyo, ushirika ndiyo hasa tiba ya kuweza kupunguza matatizo ya kilimo cha tumbaku pamoja na soko la tumbaku. *(Makofi)*

Na. 122

**Mgogoro wa Mpaka Nangaramo**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna mgogoro mkubwa wa mpaka kati ya wananchi wa kijiji cha Nangaramo Wilayani Nanyumbu na kituo cha mifugo cha ng'ombe cha Nangaramo:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwepo kwa mgogoro huo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuumaliza mgogoro huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shamba la Nangaramo lipo kilometa nne toka Masasi Mjini kandokando mwa barabara ya Masasi - Tunduru. Shamba hilo lilianzishwa kama shamba la kuzalisha mbegu ya mpunga katika miaka ya 1970. Mwaka 1982 Serikali ilibadilisha matumizi ya shamba hilo na kuwa shamba la uzalishaji mitamba chotara kwa ajili ya Mikoa ya Kusini. Shamba la Nangaramo lina eneo la hekta 6,175 na lina uwezo wa kufuga ng'ombe 2,000. Kwa sasa shamba hilo lina ng'ombe chotara 625. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1982 Serikali iliwahamisha wananchi waliokuwa wanaishi katika eneo hilo na kuwalipa fidia. Hata hivyo kutokana na mahusiano mazuri yaliyokuwepo kati ya wananchi na kituo hicho na uchache wa mifugo iliyokuwepo wakati huo baadhi ya wananchi waliruhusiwa kulima kwenye maeneo ya shamba hilo kwa kuazimwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu uliendelea kwa kipindi kirefu na hivyo yakawa mazoea ya wananchi hao kulima katika shamba hilo. Kutokana na ongezeko la mifugo mwaka 2000 Serikali iliwataka wananchi hao kuacha kulima katika shamba hilo jambo ambalo lilipingwa na baadhi ya wananchi na hivyo kuonekana kama mgogoro.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kutatua mgogoro huu Mkuu wa Wilaya ya Masasi kwa niaba ya Serikali aliitisha Mkutano wa hadhara Kijijini Nangaramo tarehe 10/11/2004 kuzungumzia suala hilo. Mkutano huo uliagiza kufanyike kikao cha usuruhishi wa kuhusisha pande zote na kuonyesha mipaka ya shamba hilo kwa vijiji vinavyozunguka. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 18/10/2005, ambapo mipaka halali ilibainika kulingana na ramani kwamba jiwe moja la mpaka liko kando kando ya barabara karibu na Mto Mbangala lenye namba 339 na lingine karibu na Mto Maselele. Pande zote mbili zilikubaliana na mipaka iliyoonyeshwa na hivyo kumaliza mgogoro uliokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuimarisha shamba la Nangaramo kama ilivyokusudiwa na kwa kutekeleza hilo katika mwaka huu wa fedha ng'ombe

majike 250 wamekwishanunuliwa ambao tayari wamekwishaanza kupelekwa shambani. Naomba Waheshimiwa Wabunge hususan Mheshimiwa Dunstan Mkapa na Wabunge wanaotoka maeneo hayo waendelee kuhamasisha ufugaji wa kisasa kwa kutumia mitamba kutoka shamba la Nangaramo. Mifugo ni uchumi, mifugo ni utajiri. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba umbali wa kutoka Masasi kwenda Nangaramo ni zaidi ya kilometa 20. Lakini pili mgogoro huu bado upo na ndiyo maana nilitumwa na wananchi kuja kulileta suala hili hapa Bungeni. *(Makofi)*

Sasa kwa kuwa wananchi wa Nangaramo hawanufaiki na Kituo hiki cha Nangaramo kwa kuwa hawana sehemu za kulima na pia kituo hiki kiliruhusu maji ya bwawa la Nangaramo kutumiwa na ng'ombe wakati huo huo wananchi wanatumia maji hayo hayo, je, Serikali sasa itafuata ule mpaka na ramani ya awali ambayo wananchi pamoja na Serikali zilikubaliana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa wananchi wa Nangaramo hawanufaiki na shughuli za ufugaji ambazo kwanza pengine wangezipata kutokana na kituo hiki kwa kuwapatia ng'ombe kwa mkopo, je, Serikali itawafaidisha vipi wananchi hao wa Nangaramo waweze kuwa na ufugaji wa kisasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama bado kuna tatizo la mpaka basi Serikali kupitia Wizara itatuma wataalam ili kusudi twende kushughulikia hili ili tuweze kumaliza tatizo lenyewe na endapo itawezekana, mimi ningependa kufika mwenyewe ili kuhakikisha kuwa nafahamu hali halisi katika kushughulikia mgogoro huu ambao unaonekana kuwa bado upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, amesema wananchi bado hawajanufaika na kuwepo kwa shamba hilo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwanza niwapongeze wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwa kuitikia wito wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ambapo sasa baadhi ya vijiji hasa vilivyokaribu na Wilaya ya Mtwara Vijijini wameshaanda Mpango wa Kopa Ng'ombe, Lipa Ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shamba la Nangaramo ndilo hilo litawezesha programu hiyo ambayo wameianzisha wananchi wa Mtwara ikiwemo Wilaya ya Masasi kuweza kupanua Mpango wa Kopa, Ng'ombe, Lipa Ng'ombe ili waweze kufaidika na uwepo wa shamba la Nangaramo na ndio azma ya Serikali kuhakikisha kuwa Mikoa ya Kusini inafaidika kuwepo kwa shamba hili ili waweze kufaidika mambo ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze vile vile Mheshimiwa Dunstan Mkapa, kwa kuwa anatetea upande mmoja suala la kilimo, lakini namwomba ageuze upande mwingine wa sarafu, mifugo. Vyote hivi vinaenda kwa pamoja na leo nashukuru sana Kilimo na Mifugo zimefuatana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa Maswali umekwisha, lakini naona sitakuwa nimewatendea haki Waheshimiwa Wabunge kwa kuyasogeza maswali manne haya yaliyopo mbele yetu hadi Mkutano wa Saba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa mamlaka niliyonayo, nitaongeza kidogo muda, tutaangalia ili tuweze kuyapunguza maswali haya kadri itakavyowezekana. Kwa hiyo, linalofuta ni la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, ambapo tumehamia sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Na. 123

**Udhibiti wa Ugonjwa wa Malaria**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa Malaria bado ni tishio kubwa kwa maisha ya Watanzania wengi nchini wakiwemo wa Liwale; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikihamasisha wananchi kutumia vyandarua vyenye ngao kama njia mojawapo ya kudhibiti Malaria:-

(a) Je, matumizi ya vyandarua vyenye ngao yalianza lini na kuna mafanikio gani?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kampeni ya matumizi ya ngao ina mwelekeo wa kibishara zaidi kuliko kudhibiti Malaria?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na mpango wa kudhibiti mazalio ya mbu Kitaifa kama njia ya kudhibiti Malaria?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya vyandarua vyenye dawa ya ngao hapa nchini yalianza rasmi mwaka 1995. Katika mikakati ya kuongeza matumizi ya vyandarua hivyo, Serikali imeweka mazingira mazuri kwa kuondoa kodi ya malighafi za kutengeneza vyandarua na kodi ya dawa ya ngao ili kuwawezesha wenye viwanda kutengeneza vyandarua vingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mpango huu umewezesha kuongezeka kwa viwanda vya kutengeneza vyandarua kutoka viwanda viwili mwaka 1997 hadi kufikia viwanda vinne mwaka 2005. Aidha, idadi ya vyandarua vilivyozalishwa nchini imeongezeka kutoka 500,000 mwaka 1997 hadi zaidi ya vyandarua 5,000,000 mwishoni mwa mwaka 2006. Kwa ongezeko hili la uzalishaji, bei ya chandarua imeshuka kutoka shilingi 7,000 mwaka 1997 hadi kufikia 3,000 hadi 5,000 mwaka 2006 (kulingana na ukubwa wa chandarua). Hatua hii imewezesha kuongezeka kwa idadi ya watumiaji wa vyandarua kwa sababu hata wananchi wenye uwezo mdogo wa kifedha walau wanaweza kumudu gharama hizi nafuu. Hadi kufikia mwaka 2005 kaya zenye angalau chandarua kimoja chenye dawa ya ngao (viuatilifu) ilikuwa ni 30.9% ikilinganishwa na 13.6% mwaka 2001. Idadi ya wanawake wajawazito wanaotumia vyandarua vyenye dawa ilifikia 22.7% kutoka 8.2% mwaka 2001. Idadi hii pia ilichangiwa na kuanzishwa kwa mpango maalum wa Hati Punguzo kwa akinamama wajawazito mwaka 2004. Aidha, idadi ya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano wanaotumia vyandarua vyenye dawa ya ngao ilifikia 23.4% kutoka 9.1% mwaka 2001. *(Makofi)*

(b) Madhumuni ya kampeni ya ngao ni kuwahamasisha zaidi wananchi kutumia vyandarua vyenye dawa ya ngao ili kuweza kujikinga na maambukizi ya ugonjwa hatari wa Malaria. Serikali itahakikisha kuwa sekta binafsi inahusishwa kikamilifu katika vita dhidi ya Malaria kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri ya uzalishaji wa vyandarua ili hatimaye kila mwananchi aweze kutumia chandarua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio dhahiri kwamba katika mpango huu wa udhibiti wa Malaria kuna mazingira ya biashara hasa ikizingatiwa kuwa wazalishaji wa vyandarua ni watu binafsi. Hata hivyo si sahihi kusema kwamba kampeni za matumizi ya vyandarua zina mwelekeo wa kibiashara zaidi kuliko kudhibiti Malaria. Naomba ifahamike kuwa lengo kuu ni kudhibiti Malaria ndio sababu kama nilivyosema hapo juu, Serikali imeweka na itaendelea kuweka mazingira zaidi ya uzalishaji wa vyandarua vyenye ngao ili kuhakikisha uzalishaji unazidi kuongezeka na kuwafikia watu wengi.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mkakati wa miaka mitano wa udhibiti wa Malaria, Serikali kupitia Mapango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria *(National Malaria Control Programme – NMCP)* imeweka kipaumbele katika uangamizaji wa mbu. Tayari mwongozo unaoelekeza njia za kuangamiza mbu umekwisha andaliwa. Njia zilizopendekezwa kutumika katika kuangamiza mbu ni kama zifuatazo:-

(i) Kuangamiza mbu wapevu na viluwiluwi kwa kutumia viatilifu *(Insecticides).*

(ii) Kuangamiza viluwiluwi kwa kulenga/ kuangamiza mazalio yao kwa kusafisha mifereji ya maji, kufukia madimbwi na mashimo yatokanayo na shughuli mbalimbali na kuhakikisha mifereji ya shambani inatengenezwa kwa namna ambayo hairuhusu maji kutuama. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Ningependa kujua nchi gani duniani ambazo zimefanikiwa kutokomeza kabisa ugonjwa wa Malaria na walitumia njia gani?

La pili, dawa ya *ALU* ambayo sasa hivi imeshaanza kutumika kwa Malaria, je, imeshaleta madhara ya aina yoyote? *Composition* yake ni nini na kama kuna *sulphur* ndani yake?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nchi nyingi zinajaribu sasa hivi kuweza kupunguza Malaria kwa kuua vimelea vya Malaria kwa kutumia viatilifu. Nchi kama Malaysia, wala hatutaki kwenda mbali, lakini Zanzibar tukiwa kama Tanzania, imeweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kuweza kupunguza matatizo ya Malaria kwa kutumia njia hii ya *indoor spraying.* Kwa hiyo, badala ya kusema ni nchi gani ya nje ambayo imefanikiwa, tuanze na mafanikio makubwa ambayo tumeyapata hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Dawa ya *ALU ...,* samahani kidogo naomba arudie lile swali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigwalilo, naomba urudie!

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ilikuwa sasa hivi imeanza kutumika dawa ya *ALU* kwa ajili ya tiba ya Malaria, je, dawa hiyo ina *composition* gani na kama ina *sulphur* ndani yake?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, *ALU* ni mkato wa dawa ya Malaria ambayo ina *combination* ya dawa *Altermethethin Lumephantrin.* Hiyo dawa ambayo inatumika kama dawa nyingine ina *desired effects* na *side effects*.

Kwa hiyo, sasa hivi tunaitumia kama dawa ya mstari wa kwanza. Tunatoa ile dawa kutokana na yule mtu anavyohitaji. Lakini kama nyingine zozote, matatizo yake yanaweza yakapatikana ni mengi yakiwemo kuumwa kichwa, kichefuchefu, kupata matatizo ya tumbo na kadhalika. Kwa hiyo, dawa hii ikitolewa kitaalam na kuzingatia kwamba unampa mgonjwa wa aina gani, basi itaweza kupunguza kwa asilimia kubwa kiasi cha matatizo ambayo hayatahitajika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Pindi Chana, naona hayupo. Tunaendelea. Linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Athuman Janguo. Mheshimiwa Janguo!

Na. 125

**Barabara ya Dar es Salaam - Morogoro kupitia Kisarawe**

**MHE. ADAM K. A. MALIMA (k.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO)** aliuliza:-

Kwa kuwa kabla ya kuanza kujengwa na kuanza kutumika barabara ya Dar es Salaam - Morogoro iliyojengwa kwa kiwango cha lami mwaka 1956, Dar es Salaam - Morogoro ziliunganishwa kwa barabara iliyopita Kisarawe - Mzenga - Ngerengere Mgudeni - Mikese - Kingolwira hadi Morogoro; na kwa kuwa hivi sasa kuna msongamano wa magari kwenye barabara ya Dar es Salaam - Morogoro:-

(a) Je, Serikali iko tayari kujenga upya barabara ya zamani kwa kiwango cha lami ili kupunguza msongamano kwenye barabara ya sasa?

(b) Kama barabara ya lami haiwezekani kwa sasa, je, Serikali iko tayari kuahidi ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe ili iweze kutumika kwa kipindi chote cha mwaka?

(c) Kwa kuwa barabara hiyo ya zamani inakatisha Mto Ruvu kati ya Mafizi na Morogoro Vijijini, Serikali haioni umuhimu ama wa kuweka kivuko au kujenga daraja ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaimarisha barabara ya kuunganisha Kisarawe na barabara kuu ya Morogoro kupitia Kiluvya - Mpuyani na vile vile barabara ya kutoka Mzenga hadi Makutano ya barabara kuu eneo la Mlandizi. Kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga barabara ya Kisarawe - Mzenga - Ngerengere - Mgudeni - Mikese, kwa kiwango cha lami.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Mzenga hadi Mlandizi imeimarishwa kwa kiwango cha changarawe na inapitika wakati wote. Barabara ya Kiluvya - Mpuyani ilikwisha jengwa kwa kiwango cha changarawe kwenye awamu ya kwanza ya kilometa 5.8 kwa msaada kutoka *DANIDA*.

Mheshimiwa Spika, tayari Mkandarasi amekwishapatikana kwa ajili ya awamu ya pili ya kilometa 14 na kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza hivi karibuni na itakamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha 2006/2007 na pindi itakapokamilika itaweza kupitika wakati wote. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna umuhimu wa kuweka kivuko au kujenga daraja katika Mto Ruvu kati ya Mafizi na Morogoro Vijijini ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali kwa sasa haina bajeti kwa kazi hiyo ila itaangalia kwa miaka ijayo kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali lenyewe hili lilikuwa linahusu kufufua barabara hii ya zamani ambayo inapitia miji mingi sana kwenye Wilaya ya Kisarawe na barabara hii pia inafanana na barabara zingine za Bagamoyo, Saadan, Pangani, Kisarawe, Manelomango, Msanga, Vikumbulo ambayo kwa asili zamani ndiyo iliyokuwa inatumika.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuna ulazima wa sasa wa kuangalia upya kufufua kwa namna yoyote ile barabara hizi ambazo zinapita kwenye miji mingi na ni ufumbuzi wa kiuchumi kwa watu wengi wa Mkoa wa Pwani?

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba Serikali itasema kuna matatizo ya bajeti, lakini kama kuna mkakati huo wa kuziangalia, ikaanza sasa hivi baina ya Serikali na Idara husika za Mkoa wa Pwani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, sisi kwenye Wizara hupokea mapendekezo ya barabara ambazo zinafaa kujengwa kutoka katika Mikoa husika kwa maana ya Bodi za Barabara za Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge kupitia Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Pwani, waweze kuleta mapendekezo namna ambavyo wanadhani barabara zingine zimepitwa na wakati na sasa kutokana na vijiji kukua maeneo mengine, basi wawe na mapendekezo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba pale ambapo kuna barabara ambazo zinakwenda *parallel* tutaangalia vile vile kama kuna barabara ambayo ipo sasa hivi inatumika, hatutaweza kukubali kulingana na vigezo vilivyopo kuwa na

barabara ambayo ni *parallel* wakati ambapo tunahitaji kujenga barabara zingine maeneo mengine. *(Makofi)*

Na. 126

**Huduma ya Simu za Mkononi - Ngara**

**MHE. PROF. FEETHAN F. BANYIKWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano ni muhimu katika kuchochea maendeleo, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mawasiliano ya simu za mkononi wananchi wa vijiji vya Murusagamba, Muganza na Mumilamila kama njia ya kuboresha mawasiliano na ulinzi katika Jimbo la Ngara?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Feethan Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango mkubwa wa huduma za simu hasa za mikononi zinazotolewa na makampuni ya simu hapa nchini. Kutokana na ukweli huo, Serikali inaendelea kuwasiliana na makampuni ya huduma za simu hususan za mkononi ili yavutiwe kuwekeza katika maeneo yote hapa nchini likiwemo Jimbo la Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* ina mpango kabambe wa kusambaza mawasiliano ya simu katika Wilaya zote Tanzania pamoja na maeneo ya vijijini. Mpango huo utaweka mtandao wa mitambo inayotumia teknolojia ya *Code Division Multiple Access (CDMA)*. Awamu ya kwanza ya utekelezaji ilianza mwishoni mwa mwaka 2006 kwa kujenga mitambo ya kurushia simu maeneo yote ya miji mikuu ya mikoa, Wilaya na baadhi ya maeneo ya vijijini. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango huu unategemea kumalizika mwezi Desemba, 2007. Utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango huu utaendelea mwaka 2008 na unategemea kusambaza mtandao wa *Code Division Multiple Access (CDMA)* katika maeneo mengi ya vijijini vikiwemo vijiji vya Murusagamba, Mumilamila na Muganza Wilayani Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kampuni ya *toGO*, mwaka huu wanategemea kufikisha mawasiliano ya simu maeneo ya Ngara Mjini, *Rulenge Mission, Rusumo Border,* Nyakahara, Benako na *Kabanga Nickel.* Baada ya kujenga minara katika maeneo hayo, watafanya tathmini kuona kama maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yanapata mawasiliano. Kama itaonekana kuwa hayapati, watahakikisha wanafikisha mawasiliano hayo mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kampuni ya Simu ya *Vodacom* imeshafanya tathmini katika eneo la Muganza. Ujenzi wa mnara utafanyika baada ya bajeti ya kampuni hiyo kupitishwa. Kampuni hiyo imeahidi kufanya utafiti katika maeneo ya Murusagamba na Mumilamila siku za karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa kampuni ya simu ya *Zantel,* watafikisha mawasiliano hayo kwa kutumia minara itakayowekwa na *Vodacom.*

Kampuni ya Simu ya *Celtel* imepanga kufikisha mawasiliano ya simu Murusagamba ifikapo mwezi Julai, 2007. Kampuni hiyo inatarajiwa kufikisha mawasiliano Muganza na Mumilamila mwaka kesho yaani mwaka 2008. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tuendelee! Kwanza majibu yanatosheleza, ni mazuri na mimi sitashangaa kama katika mabadiliko yajayo ya Baraza la Mawaziri, Naibu huyu naye akapanda! Nayasema haya kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Na. 127

**Ujenzi wa Shule za Sekondari kila Kata**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Geita imefaulu kujenga shule za sekondari kwa kila Kata kutokana na juhudi za wananchi wake ambao wameitikia wito wa Serikali na Ilani ya Uchaguzi iliyosema kuwa ifikapo mwaka 2010 kila Kata itakuwa na shule ya sekondari.

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni jambo la kujivunia na kuwapa moyo wananchi wa Geita kwa kuwasaidia majengo mengine?

(b) Je, kwa nini Serikali isipeleke walimu wa kutosha katika sekondari hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatvyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona fahari na ni jambo la kujivunia kwa wananchi wa Geita kuitikia wito wa Serikali na Ilani ya Uchaguzi na kuwezesha Wilaya hiyo kufaulu kujenga shule ya sekondari kila Kata, nawapongeza sana.

Kwa utaratibu wa sasa, Mkoa ndio unaopeleka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi mapendekezo ya matumizi ya fedha za *MMES* kwa kila Wilaya na shule husika. Uamuzi unapaswa kuwashirikisha viongozi na wadau wa elimu katika Mkoa na Wilaya. Hivyo, Mkoa kwa kushirikiana na Wilaya wataamua kipaumbele wanachotaka kujenga. Serikali itaendelea kuwaunga mkono wananchi wa Geita kwa kuchangia katika ujenzi wa majengo ya shule kadri fedha zatakapopatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikizipatia shule za Wilaya ya Geita walimu kadri walivyopatikana ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu. Mwaka 2004/2005 jumla ya walimu 86 walipangwa Wilaya ya Geita. Walimu 73 kati ya hao walikuwa wa Stashahada na 13 wa cheti. Mwaka 2006/2007 jumla ya walimu 252 wamepangwa Mkoa wa Mwanza ambao watapangwa katika Wilaya zote za Mkoa wa Mwanza ikiwemo Wilaya ya Geita. Serikali itaendelea na jitihada za kuwapata walimu

na kuwapanga katika Mkoa wa Mwanza na hatimaye Wilaya ya Geita hadi ikama ya walimu katika shule zake itakapokamilika.

Hata hivyo, Serikali inatoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa kushirikiana na wananchi kujenga nyumba za walimu za kutosha ili kuweka mazingira mazuri kwa walimu watakaopangwa huko kufanya kazi zao kwa utulivu, amani na ufanisi zaidi. Ahsante! *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tufike mwisho, Maswali yamekwisha. Namwomba radhi Mheshimiwa Ernest Mabina, kwamba haikuwezekana kutimiza haki yake ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini muda kwa kweli umetutupa mkono. *(Makofi)*

Matangazo, naomba Waheshimiwa Wabunge tutambue pale *Speaker's Gallery* uwepo wa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utangazaji Tanzania, Bwana Dunstan Tido Mhando. Dunstan Karibu nyumbani. Watu wengi wenye uwezo na vipaji kama vyako huzamia huko huko, lakini wewe baada ya mafanikio makubwa *BBC London,* kiasi cha miaka uliyokaa umeamua kurudi nyumbani. Karibu sana na Watanzania tunatazamia kazi nzuri sana kwako. Ahsante sana! Karibu sana! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia kwenye *Speaker's Gallery*, Spika ana mgeni wake ambaye ni Katibu wangu katika Jimbo kule Urambo Mashariki. Huyo kijana anaitwa Paulo Shija. Anafanya kazi nzuri, amekuja kuchukua silaha zaidi za kuendeleza maendeleo Jimboni. Unajua haya Majimbo haya usipoyalea inakuwa taabu kidogo na lazima kuyapalilia mapema. Ahsante sana Paulo kwa kazi nzuri unayonifanyia. *(Makofi/Kicheko).*

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, nimtambulishe mgeni wake Mwalimu Bakari, Mkufunzi wa Chuo cha Ualimu Ilonga, Morogoro. Karibu sana Mwalimu.

Pia kutakuwa na Mkutano leo wa Naibu Mawaziri wote kukutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Pinda na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambaye jina lake mnalifahamu. Watakutana katika Ukumbi Namba 231 mara tu baada ya Bunge kuahirishwa.

Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya Bunge kuahirishwa Naibu Mawaziri watakutana na Mawaziri wawili katika ukumbi umerekebishwa, siyo 231 tena! Basi badala ya 231, Naibu Mawaziri na Mawaziri wawili watakutana baada ya Bunge kuahirishwa Ukumbi wa Pius Msekwa. *(Makofi)*

Pia nimepata tangazo hapa kwamba kesho kutakuwa na hafla ya kuchangia ujenzi wa Chuo Kikuu kipya kinachoandaliwa cha Kanisa la Anglikana pale iliyokuwa shule ya Sekondari ya Mazengo. Mgeni rasmi aliyealikwa ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na hafla itaanza saa tatu asubuhi. Nadhani kwa wale wote ambao tutakuwa tuko bado Dodoma itakuwa ni jambo zuri ili kuweza kumuunga mkono Rais wetu katika tukio hilo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mohammed Misanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ameniomba nitangaze kuwa mara baada ya kuahirishwa Bunge, wajumbe wote wa

Kamati ya Miundombinu wakutane Ukumbi namba 133 kwa ajili ya kupitia rasimu ya ratiba ya shughuli za Kamati kwa mwezi Machi - Aprili. Wajumbe wote Kamati ya Miundombinu Ukumbi namba 133 mara baada ya kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Uwekezaji na Biashara, anaomba wajumbe wa Kamati Ndogo ya Uwekezaji na Biashara wawe na kikao leo saa 6.00 mchana ukumbi namba 227 na Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara...oh..

Sasa hizi mbili moja ni ndogo na nyingine nadhani ndiyo Kamati kamili, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara wakutane mara baada ya Bunge kuahirishwa leo katika Ukumbi namba 219. Kwa hiyo, Kamati ya Uwekezaji na Biashara mara baada ya Bunge kuahirishwa. Huo ndio mwisho wa matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna Muswada wa kusomwa mara ya kwanza. Samahani.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Ulisomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kutunga Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa *(A Bill for an Act to Provide for Prevention and Combuting Corruption)***

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza)*

**SPIKA:** Ahsante! Muswada huo umesomwa kwa mara ya kwanza, tutauzingatia katika Mkutano wa Bunge ujao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hadi hapo nadhani ndio tunafikia karibu mwisho, maana yake tukio la Waziri Mkuu ndiyo huwa la mwisho kufikia mwisho wa shughuli zetu hizi za Mkutano wa Sita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tatizo la Mheshimiwa Chacha Wangwe. Katika uamuzi wangu niliutoa hapa Bungeni siku ya Alhamisi tarehe 1 Februari, 2007 kuhusu uthibitisho wa kauli ya Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mbunge wa Jimbo la Tarime, aliyoitoa Bungeni Tarehe 10 Julai, 2006.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mambo mengine niliekeza kwamba Mheshimiwa Chacha Wangwe asichukuliwe hatua za kuadhibiwa na Bunge, badala yake nilimtaka aisahihishe kauli yake aliyoitoa Bungeni tarehe 6 Julai, 2006 iliyodai kwamba mauaji ya Tarime mwaka 2005 yalikuwa ni ya kisiasa yakilenga kumzuia yeye kuchaguliwa kuwa Mbunge, kitu ambacho si kweli. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapa si kwamba tunakataa kwamba hakukua na mauaji Tarime, kumekuwa na mauaji Tarime hata mwaka jana, sasa sijui nayo hayo ni ya kumzuia, hata mwaka huu, sijui hayo ni ya kumzuia asifanye kazi! Sielewi! Kwa hiyo, nisema tu Mheshimiwa Chacha Wangwe, juzi alikuja ofisini kunishukuru kwa uamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, ni kwa mshangao mkubwa kwamba jana hata baada ya mimi kukumbusha kwamba anahitajika, kitu cha kiungwana tu cha kusahihisha kauli, hataki! Ameleta barua eti anaomba atoe maelezo binafsi.

Baada ya uamuzi wa Spika, yeye anataka atoe maelzo binafsi ambayo hayapo kwenye utaratibu wa Bunge letu au Bunge lolote la *Commonwealth*. Pia ameathiri Kanuni ya 50 ambayo inakataza kwa maeneo yafuatayo: "Itakuwa ni marufuku kwa Mbunge yeyote katika majadala wowote Bungeni kuzungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Wabunge, Majaji na kadhalika."

Waheshimiwa Wabunge, yeye katika barua yake ambayo ni ndefu mno, siwezi kuisoma hapa, anajaribu kuhoji mwenendo wangu. Katika maelezo yake hayo binafsi aliyoomba nimruhusu ayatoe hapa Bungeni, Mheshimiwa Chacha Wangwe, kwa dhahiri kabisa anapinga uamuzi wangu nilioutoa hapa Bungeni tarehe 1 Februari, 2007 kuhusu suala lake nililokwisha kulitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chacha Wangwe haishii hapo tu, bali katika maelezo yake hayo anajaribu kunielekeza uamuzi ambao yeye anadhani ningepaswa kuutoa kuhusiana na suala lake. Kimsingi ni kwamba Mheshimiwa Wangwe anapinga uamuzi wangu nilioutoa hapa Bungeni na kuhoji mwenendo wangu kama Spika.

Nataka ieleweke kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwamba uamuzi wa Spika ndani ya Bunge ni sawa na hukumu ya Jaji wa Mahakama na kama ilivyo kwa hukumu za Mahakama, upo utaratibu wa Rufaa ambao umezingatiwa katika Kanuni zetu, Kanuni ya 4(3) ambayo inasema kwamba nanukuu: "Spika atawajibika kutilia nguvu Kanuni zote za Bunge na endapo Mbunge yeyote hataridhika na uamuzi wa Spika, anaweza kuwasilisha sababu za kutoridhika kwake kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni za Bunge ambayo itatakiwa ikutane mara moja kufikiria na kutoa uamuzi wake kwa Spika, juu ya jambo hilo na Spika atalijulisha Bunge uamuzi huo uliotolewa, isipokuwa Spika hatakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni wakati inapojadili jambo linalomhusu." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chacha Wangwe hakuifuata kanuni hii. Kwa hiyo, hakufuata utaratibu uliowekwa na kanuni. Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Chacha Wangwe hakufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni za Bunge na kwa kuwa Mheshimiwa Wangwe anaomba nimruhusu atoe maelezo binafsi, ambayo yamepigwa marufuku chini ya Kanuni 50(6), ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Chacha Wangwe, amekaidi kwa makusudi kutekeleza maelekezo ya Spika niliyoyatoa hapa Bungeni kuhusiana na suala lake, yaani kusahihisha kauli aliyoitoa Bungeni tarehe 6 Julai, 2006 kabla ya Mkutano wa Sita kumalizika. *(Makofi)*

Kitendo hiki ni utovu mkubwa wa nidhamu. Kutokana na ukiukwaji dhahiri wa kanuni za Bunge na ubabe alioudhihirisha Mheshimiwa Chacha kwa kuanzisha malumbano na Spika, kinyume cha utaratibu wa Mabunge, pamoja na hili letu ninaagiza kwamba, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, ikutane leo mara baada ya Mkutano huu kuahirishwa ili kumchukulia hatua siyo kujadili. Hakuna tena kujadili hukumu iliyochukuliwa ili kumchukulia hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na Sheria Na. 3 ya mwaka 1988. Ahsante sana. *(Makofi)*

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Sita wa Bunge lako Tukufu umehitimisha shughuli zote zilizokuwa zimepangwa. Mkutano huu ni wa kwanza baada ya Serikali ya Awamu ya Nne kutimiza mwaka mmoja madarakani. Taarifa za mafanikio na changamoto zilizojitokeza zimewasilishwa kupitia Mikutano mbalimbali ya Chama Tawala, Serikali na kwenye vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, nachukua nafasi hii, tena kwa niaba ya Serikali na wafanyakazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kutoa rambirambi zetu kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa familia, jamaa na marafiki kwa msiba uliotokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge na Uratibu Marehemu Juma Jamaldin Akukweti. Wote tulimfahamu Marehemu Akukweti kwa umakini na umahiri wake hapa Bungeni. Marehemu Akukweti alifariki kutokana na ajali ya ndege iliyokuwa inamrejesha Dar es Salaam baada ya kumaliza kazi ya kukagua Soko la Mwanjelwa, lililoteketea kwa moto Mkoani Mbeya.

Katika ajali hiyo, Watumishi wa Serikali walipoteza maisha. Watumishi hao ni Bibi Theresia Nyantori, Mwandishi wa Habari wa Idara ya Habari, Bwana Nathaniel Katinila, Mratibu wa Mradi wa Masoko na Bwana George Bendera - Afisa Habari, Idara ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu. Majeruhi katika ajali hiyo ambao bado wanapata matibabu lakini wametoka Hosptali ni Bwana Nisetas Kanje, Katibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Rubani wa Ndege hiyo Bwana Martin Sumari. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awasaidie majeruhi wote waweze kupona haraka na kurudia katika afya zao.

Napenda pia kupitia Bunge lako Tukufu kutoa salaam za rambirambi na pole nyingi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu waliopoteza maisha yao katika maafa na ajali zilizotokea sehemu mbalimbali nchini. Tuwaombee Marehemu wote ili Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alimteua Mheshimiwa Dr. Batilda Burian - Mbunge wa Viti Maalum, kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Vile vile Mheshimiwa Bernard Membe, aliteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuchukua nafasi ya Dr. Asha-Rose Migiro, ambaye ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Aidha, Mheshimiwa William Ngeleja - Mbunge wa Sengerema, aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Gaudence Kayombo - Mbunge wa Mbinga Mashariki, aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda tena kumpongeza Dr. Asha-Rose Migiro kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Kuteuliwa kwake kushika wadhifa huo mkubwa duniani ni kielelezo thabiti cha kuheshimika kwa mchango wa Tanzania katika duru za Kimataifa. Hii ni sifa kubwa kwa nchi yetu na Bara zima la

Afrika na nchi zote zinazoendelea duniani. Tunamtakia Dr. Asha-Rose Migiro afya njema ili aweze kutekeleza majukumu aliyokabidhiwa kwa umahiri na umakini. *(Makofi)*

Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum, kuchukua nafasi ya Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, jumla ya Maswali 127 ya Msingi na mengine mengi ya nyongeza ya Waheshimiwa Wabunge, yamejibiwa na Serikali. Miswada tisa imesomwa kwa Mara ya Kwanza na kujadiliwa. Baadhi ya Miswada hiyo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Usajili wa Biashara wa mwaka 2006. Muswada huu utawezesha kubadilisha utaratibu wa sasa wa utoaji wa leseni za biashara isipokuwa leseni za udhibiti, ambazo zitaendelea kutolewa na mamlaka husika kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii mpya itaboresha mazingira ya kuanzisha na kufanya biashara na kuwawezesha wafanyabiashara walioko katika sekta isiyo rasmi kurasimisha biashara zao.

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuweka Misingi na Taratibu za Mishahara, Posho, Marupurupu na Maslahi mengine ya Majaji ya mwaka 2007, aidha kuna Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo Tanzania wa mwaka 2007. Kupitishwa kwa Miswada hii miwili kutasaidia kuboresha na kuimarisha shughuli za Mahakama na vyombo vyake.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada wa Sheria ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2007 yapo marekebisho ya sheria kumi (10) ambazo Bunge lako Tukufu limeyapitisha. Marekebisho ya Sheria hizo yana lengo la kuboresha huduma za Mahakama zinazohusiana na matumizi ya Sheria za mwenendo wa makosa ya jinai, fedha haramu na makosa yanayohusu utaifishaji wa mali haramu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yatapanua uwigo wa matumizi wa sheria hizi ikiwa ni pamoja na utumishi wa Mahakama.

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari wa mwaka 2007: Kurekebishwa kwa Sheria hii kunatoa nafasi ya matumizi mazuri ya Bahari kwa kulinda maslahi ya wavuvi wetu na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia limeridhia maazimio manne kuhusu Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu Kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika.

Marekebisho katika Mkataba wa Kuanzisha Shirikisho la Afrika ya Mashariki, Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Usimamizi wa Taka za Sumu na nyinginezo na Mkataba wa Shirika la Afya Duniani kuhusu Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku, Miswada yote pamoja na Maazimio haya yamejadiliwa kwa kina na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya siku zote za Mkutano huu. Aidha, nawashukuru kwa michango yenu wakati wa kujadili taarifa mbalimbali za Kamati za Kudumu za Bunge zilizowasilishwa hapa Bungeni. Mjadala ulikuwa wa kina na uliojenga hoja za kuishauri Serikali namna ya kurekebisha kasoro zilizoonekana na Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itazingatia ushauri huo kadiri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Mvua na Athari kwa Miundombinu, katika msimu wa mwaka 2006/2007, maeneo mengi nchini yamepata mvua nyingi. Takwimu za Mamlaka ya Hali ya Hewa, zinaonyesha kuwa katika msimu wa mwaka jana, yaani 2005/2006, kiwango cha juu cha mvua kilichotolewa taarifa ni milimita 428.5 katika Kituo cha Bukoba na kiwango cha chini ni milimita 48.4 katika Kituo cha Morogoro.

Katika msimu huu wa mwaka 2006/2007, kiwango cha juu kilichofikiwa hadi sasa ni milimita 946.0 katika Kituo cha Bukoba na kiwango cha chini ni milimita 308.3 katika Kituo cha *KIA*. Katika Maeneo ya Kibena Wilayani Njombe, hadi mwishoni mwa Januari, 2007, walirekodi milimita 707 za mvua, ambazo zinakaribia milimita 744 za mvua iliyorekodiwa msimu wote uliopita wa mwaka 2006.

Aidha, katika baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Rungwe, kati ya Septemba na Desemba mwaka 2006 zilirekodiwa milimita 640 za mvua ambazo ni karibu mara mbili ya milimita 384 zilizorekodiwa Septemba hadi Desemba 2005. Hii ni habari njema sana kwa wakulima wa mazao yanayolimwa katika nyanda za juu. Kwa jumla taarifa zinaonyesha kuwa nchi yetu imepata mvua ya juu ya wastani katika maeneo mengi nchini. *(Makofi)*

Kiwango hicho cha mvua katika msimu huu kinakaribia sana kiwango cha mvua wakati wa *El-Nino* ya mwaka 1997/1998. Kiwango cha juu cha mvua za *El-Nino* ya mwaka 1997/1998, kilifikia milimita 1,340.6 katika Kituo cha Tanga, wakati kiwango cha chini kilikuwa milimita 371.6 katika Kituo cha *KIA*. Wataalam wa Hali ya Hewa wameeleza kuwa kumekuwa na hali ya *El-Nino* ambayo pamoja na vimbunga katika Bahari ya Hindi imesababisha ongezeko la mvua tangu Oktoba mwaka 2006. Japo mvua za msimu huu bado hazijafikia mvua hizo za *El-Nino*, katika baadhi ya maeneo, zimeanza kusababisha athari kubwa kwa mali za wananchi na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa za wananchi kupoteza maisha, uharibifu wa makazi na miundombinu. Kwa mfano, katika kipindi cha siku tano, kati ya tarehe 01 na 06 Februari, 2007 katika barabara ya Manyoni hadi Singida, maeneo ya Idabaganje na Kamenyanga, kumejitokeza chemchem chini ya ardhi iliyoharibu barabara na hivyo magari kukwama na kushindwa kuendelea na safari. Takriban magari yapatayo 880 yalikuwa yamekwama barabarani katika maeneo hayo na mengine 100 katika Mji wa Manyoni. Hata hivyo, kutokana na juhudi zinazoendelea za matengenezo ya sehemu hizo, magari yameanza kupita. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuwezesha usafiri kwa njia ya barabara hiyo na nyingine nchini kurejea katika hali ya kawaida mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia wananchi kwamba, Serikali imeajiri Kampuni ya *Konoike* ambayo kazi yake ni kuondoa magari yaliyokwama katika maeneo hayo ya Singida. Napenda kuwahakikishia wananchi kwamba Serikali wakati wote itaendelea kuchukua hatua zinazopasa kurejesha huduma zinazoharibika na kutoa misaada ya dharura pale inapolazimu. Aidha, natoa wito kwa wananchi wenye makazi yao mabondeni kuwa wachukue hatua za tahadhari za kujihami na mafuriko yanayoweza kutokea. *(Makofi)*

Pamoja na matatizo yaliyojitokeza, mvua hizi zimeleta neema na matumaini makubwa kwa wakulima yetu. Hali ya mazao mashambani katika maeneo mengi nchini ni nzuri. Mabwawa makubwa ya kuzalisha umeme yameanza kujaa. Taarifa zinaonyesha kuwa Mto Ruaha Mkuu umejaa maji kwa mara ya kwanza katika kipindi cha takriban miaka minne iliyopita. Mto huu na mingine ndiyo inayotiririsha maji kuelekea Bwawa la Mtera na Kidatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana usiku nilipigiwa simu na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara anasema, Mto Ruvuma pia umejaa na umeanza kusababisha mafuriko. Mto Ruaha Mkuu na mingine ndiyo inayotiririsha maji kuelekea Bwana la Mtera na Kidatu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kipindi hiki, mwaka 2006 maji katika Bwawa la Mtera yalifikia kina cha meta 689.09 tu. Mwaka huu 2007 hadi tarehe 8 Februari, maji yalikuwa yamefikia kina cha meta 697.59. Kiwango hiki kinakaribia kiwango cha juu kabisa cha uwezo wa bwawa cha meta 698.5. Taarifa za wataalam zinaeleza kuwa hadi tarehe 8 Februari, maji yalikuwa yanaingia bwawani kwa kasi ya meta za ujazo 752 kwa sekunde. Kwa hali hii sasa *TANESCO* wanaweza kuanza kutumia bwawa hili kuzalisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu, imefanya tathmini ya awali ya uharibifu uliotokea na gharama za kufanya matengenezo. Uharibifu huo umehusisha jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa 6,440 ambazo baadhi zinapitika kwa shida au hazipitiki kabisa. Tathmini pia inaonyesha kuwa baadhi ya miundombinu ya viwanja vyetu vya ndege imeharibiwa na mvua. Viwanja vilivyoathirika zaidi ni vile vya Mwanza na Shinyanga ambavyo sehemu za njia za kurukia na kutua ndege zimeharibiwa.

Pia, mafuriko yameathiri madaraja, mifumo ya maji na barabara zinazoingia na kutoka katika viwanja hivyo. Aidha, miundombinu mingine iliyoharibiwa ni ya usafiri wa majini ambapo bandari za Mwanza na Kigoma, zimeathirika kwa kujaa mchanga, hivyo kupunguza kina cha maji. Uharibifu pia umetokea katika Reli ya *TAZARA* ambapo makalvati kati ya Stesheni ya Kurasini na Yombo yameharibika vibaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya tathmini ya kina, Wakala wa Barabara *(TANROADS)* amekadiria kuwa zitahitajika jumla ya Shilingi bilioni 10.4 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya dharura ya kuwezesha barabara hizo zipitike angalau kwa muda. Aidha, ili kufanya matengenezo ya kurejesha barabara zilizoathirika katika hali yake ya kawaida zinahitajika Shilingi bilioni 45.1.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanja vya ndege, vitahitaji Shilingi milioni 937 kwa ajili ya kuvirejesha katika hali yake ya kawaida. Serikali inaendelea kuchukua hatua za dharura za kurejesha baadhi ya miundombinu iliyoharibika katika hali yake ya kawaida. Lengo ni kurejesha mawasiliano kwa haraka ili huduma na shughuli

mbalimbali za wananchi zisiathirike. Kwa upande wa ukarabati wa njia za reli za kati *(TRC)* na *TAZARA*, hadi sasa matengenezo ya dharura yamekwishafanyika na kuwezesha kurejesha huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, uzingatiaji wa misingi ya Utawala Bora katika Halmashauri, Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wanajadili Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, wamezungumzia mambo mengi kuhusu Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kwa muhtasari hali ya kiwango cha uzingatiaji wa Misingi ya Utawala Bora katika Halmashauri zetu. Tangu Serikali ilipoanza kutekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa, mwaka 2000, limekuwepo zoezi la kufuatilia kiwango cha uzingatiaji wa misingi ya Utawala Bora katika maeneo yafuatayo:-

Demokrasia, ushirikishwaji wa jamii, utawala wa sheria, uadilifu wa Viongozi na Watendaji katika Halmashauri, uwazi na uwajibikaji, ufanisi katika utendaji katika ngazi zote za Halmashauri, uzingatiaji wa masuala ya jinsia, utaratibu wa upangaji mipango, stadi za upangaji mipango na matumizi ya takwimu katika kuandaa mipango. *(Makofi)*

Uchambuzi uliofanywa na *TAMISEMI* mwaka 2006 katika kufuatilia uzingatiaji wa vigezo hivyo vya Utawala Bora katika Halmashauri mbalimbali nchini, umeonyesha kwamba kumekuwepo na mafanikio ya kuridhisha ikilinganishwa na mwaka 2000.

Hata hivyo, kuna baadhi ya Halmashauri, ambazo ziko nyuma katika kuzingatia misingi ya Utawala Bora. Baadhi ya Halmashauri, ambazo zilikuwa zimekwishaanza kuzingatia misingi ya Utawala Bora kwa kiwango cha juu zimeanza kushuka. Uchambuzi wa kigezo kimoja kimoja kwa baadhi ya Halmashauri ni kama ifuatavyo:

Uzingatiaji wa Demokrasia: Katika mwaka 2002, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga iliongoza katika eneo hili kwa asilimia 93 na Halmashauri za mwisho zilikuwa ni Manispaa ya Kinondoni na Tanga ambazo zilikuwa na asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, upimaji uliofanyika mwezi Juni, 2006, umeonyesha kuwa Halmashauri zilizokuwa zinaongoza ni Manispaa ya Mtwara Mikindani na Manispaa ya Morogoro zenye asilimia 95 kila moja na Halmashauri za mwisho ni Halmashauri ya Mji wa Lindi yenye asilimia 73 na Mafia yenye asilimia 74.

Ushirikishwaji wa Jamii: Katika mwaka 2002, Halmashauri iliyokuwa inaongoza katika eneo hili ni ya Wilaya ya Singida, iliyokuwa na asilimia 90 na Halmashauri ya mwisho ilikuwa ni ya Wilaya ya Simanjiro ambayo ilikuwa na asilimia moja tu. Mwezi Juni, 2006, Halmashauri zilizokuwa zinaongoza ni Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani asilimia 77 na Manispaa ya Temeke asilimia 76. Halmashauri za mwisho zilikuwa Mafia asilimia 50 na Tandahimba asilimia 53. *(Makofi)*

Utawala wa Sheria: Katika mwaka 2002, Halmashauri iliyokuwa inaongoza katika eneo hili la Utawala wa Sheria ni ya Wilaya ya Kasulu iliyokuwa na asilimia 93; na Halmashauri za mwisho zilikuwa za Wilaya za Babati, Kiteto na Simanjiro zikiwa na asilimia 20 tu. Mwezi Juni, 2006, Halmashauri iliyokuwa ikiongoza ni Nachingwea ikiwa na asilimia 98 na za mwisho ni Pangani na Ulanga zikiwa na asilimia 50. *(Makofi)*

Uadilifu wa Viongozi na Watendaji: Mwaka 2002, Halmashauri ambayo ilikuwa inaongoza ni Shinyanga ambayo ilikuwa na asilimia 85 na ya mwisho ilikuwa ni Manispaa ya Kinondoni yenye asilimia 11. Mwezi Juni, 2006. Halmashauri zilizokuwa zinaongoza katika kigezo hiki ni Halmashauri za Wilaya ya Mtwara na Masasi zikiwa na asilimia 99 kila moja na ya mwisho ilikuwa ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ikiwa na asilimia 43. *(Makofi)*

Uwazi na Uwajibikaji: Mwaka 2002, Halmashauri iliyokuwa ikiongoza katika kigezo hiki ni Wilaya ya Shinyanga ikiwa na asilimia 100 na ya mwisho ilikuwa ni Manispaa ya Tanga ikiwa na asilimia 16. Mwezi Juni, 2006. Halmashauri iliyokuwa inaongoza ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, ikiwa na asilimia 94 na mwisho ni Kiteto ikiwa na asilimia 27. *(Makofi)*

Ufanisi wa Utendaji Kazi: Mwaka 2002, Halmashauri iliyokuwa inaongoza ni Halmashauri ya Mji wa Lindi, ikiwa na asilimia 72 na mwisho ilikuwa ni Manispaa ya Kinondoni ikiwa na asilimia 13 tu. Mwezi Juni, 2006, Halmashauri iliyokuwa inaongoza katika eneo hili la ufanisi na utendaji kazi ni Manispaa ya Morogoro ikiwa na asilimia 72; na mwisho ni Halmashauri ya Wilaya ya Tarime yenye asilimia 41. *(Makofi)*

Uzingatiaji wa Jinsia: Mwaka 2002, Halmashauri zilizokuwa zinaongoza ni Manispaa ya Tabora na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, ambazo zilikuwa na asilimia 80 kila moja; na Halmashauri ya mwisho ilikuwa ni Simanjiro iliyokuwa na asilimia tano tu. Mwezi Juni, 2006, Halmashauri zilizokuwa zinaongoza ni Halmashuri ya Lushoto ikiwa na asilimia 82 na Kahama asilimia 70; Halmashauri za mwisho ni pamoja na Tunduru asilimia 10, Misungwi asilimia 12 na Mbozi na Chunya zenye asilimia 15 kila moja. *(Makofi)*

Utaratibu wa Upangaji Mipango: Mwaka 2002, Halmashauri ambayo ilikuwa inaongoza ni ya Wilaya ya Singida ikiwa na asilimia 95 na mwisho ni Jiji la Mwanza lililokuwa na asilimia sifuri (0). Mwezi Juni, 2006, Halmashauri ambazo zilikuwa zinaongoza katika Utaratibu wa Upangaji Mipango ni pamoja na Masasi asilimia 100, Manispaa ya Iringa na Temeke asilimia 93 kila moja na Halmashauri za Wilaya za Bariadi na Kahama nazo zikiwa na asilimia 93. Halmashauri za mwisho katika utaratibu wa upangaji wa mipango ni pamoja na Magu, Tarime na Jiji la Mwanza zote zikiwa na asilimia 50. *(Makofi)*

Stadi za Upangaji wa Mipango: Halmashauri iliyokuwa inaongoza mwaka 2002 ni ya Wilaya ya Monduli ikiwa na asilimia 100 na Halmashauri za mwisho zilikuwa za Wilaya ya Shinyanga na Mji wa Musoma ambazo zote zilikuwa na asilimia sifuri (0). Mwezi Juni, 2006, Halmashauri ambazo zilikuwa zinaongoza ni pamoja na Monduli, Kiteto, Simanjiro, Iringa na Mbinga, zote zikiwa na asilimia 100 na Halmashauri za mwisho ni Mkuranga, Bagamoyo, Kibaha na Halmashauri ya Mji wa Korogwe zikiwa na asilimia 70 kila moja. *(Makofi/Kicheko)*

Kigezo cha mwisho, Matumizi ya Takwimu katika Mipango: Katika mwaka 2002, Halmashauri iliyokuwa inaongoza ni ya Wilaya ya Masasi ikiwa na asilimia 94 na ya mwisho ni ya Wilaya ya Babati ikiwa na asilimia 25. Mwezi Juni, 2006, Halmashauri zilizokuwa zinaongoza katika matumizi ya Takwimu katika Mipango ni pamoja na Magu

asilimia 93, Kilosa na Ulanga zikiwa na asilimia 90 kila moja; na Halmashauri ya mwisho ilikuwa Korogwe ikiwa na asilimia 72. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu hizo kwa haraka, tunaona kwamba Halmashauri nyingi zinazingatia kwa wastani misingi ya Utawala Bora, kwa vigezo nilivyovitaja. Aidha, kwa Halmashauri ambazo zinashindwa kutimiza vigezo vya Utawala Bora kwa zaidi ya asilimia 60 ni dhahiri kwamba katika Halmashauri hizo kuna kero nyingi na hili sio jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge hawalifahamu kwa sababu mnatoka katika maeneo hayo na sisi wote tuliopo hapa ni Madiwani kwa mujibu wa sheria.

Kwa hiyo, napenda kutoa wito kwenu Waheshimiwa Wabunge, twende kufuatilia uzingatiaji wa misingi ya Utawala Bora, katika Halmashauri zetu ili kuhakikisha wananchi wanahudumiwa ipasavyo. Jambo la uzingatiaji wa misingi ya Utawala Bora katika kutekeleza shughuli za Halmashauri ni muhimu sana katika kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM wa mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuzipongeza Halmashauri zilizofanya vizuri katika zoezi hili. Kwa Halmashauri ambazo zimepata alama zisizoridhisha, zinao wajibu wa kuchukua hatua za haraka kuongeza juhudi za kuboresha maeneo yenye udhaifu ili kuimarisha dhana ya utawala bora nchini. Serikali kwa upande wake, imechukua hatua za kuwezesha Halmashauri kuajiri watumishi wenye ujuzi na utaalam. Hata hivyo, bado lipo tatizo la wataalam kutokupenda kufanya kazi katika baadhi ya Halmashauri au baadhi ya Halmashauri au Mikoa nchini.

Kwa mfano, kati ya Wahasibu 461 walioajiriwa katika Halmashauri 121 mwaka 2006, Wahasibu 192, sawa na asilimia 41.6 hawajaripoti katika Vituo vyao vya kazi walivyopangiwa. Aidha, kati ya Wakaguzi wa Ndani 179 waliopangiwa kazi, Wakaguzi 90, sawa na asilimia 50.3 hawajajitokeza katika Halmashauri hizo. Hata hapa Dodoma pamoja na kuwa ni Mji unaokua na wenye mawasiliano ya uhakika, bado wataalam hawataki kufanya kazi hapa.

Kwa mfano, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dodoma ilitangaza nafasi 17 za wataalam wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya kisasa, lakini hadi sasa waliopatikana ni wataalam watatu (3) tu. Waombaji wengi waliofanyiwa usaili hasa wale wanaoishi Dar es Salaam wanasema hawapendi kufanyia kazi hapa Dodoma.

Vilevile, mwaka 2006/2007, Ofisi ya Waziri Mkuu -*TAMISEMI* ilitangaza nafasi za ajira 138, lakini waombaji wenye sifa waliojitokeza, kufaulu usaili na kukubali ajira ni 89 tu. Kwa msingi huo, pamoja na Serikali kusubiri mapendekezo ya namna ya kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma, kila Halmashauri na Taasisi ya Umma inayo changamoto ya kuona ni kwa jinsi gani inaweza kuwa na vivutio maalum vya kuwawezesha wataalam wabaki kwenye ajira katika maeneo yao. Napenda kuwapongeza sana Waalimu wote nchini ambao wao wanakubali ajira katika sehemu yoyote katika nchini yetu. Nawaomba wataalam wengine waige mfano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zoezi hili la uzingatiaji wa misingi ya Utawala Bora katika Halmashauri zetu linatupa changamoto mbalimbali. Tukiendelea kutumia utaratibu huu

wa tathmini za mara kwa mara tutaweza kuzisaidia Halmashauri zetu kwenda kwa kasi na kuongeza ufanisi na uwajibikaji wake kwa wananchi. Aidha, tutaziwezesha kupanua na kuboresha huduma muhimu kwa wananchi, hivyo kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, upimaji huu, vilevile unaongeza ushindani wa maendeleo kwani Halmashauri zinazofanya vizuri zinafuzu kupata Ruzuku ya Fedha za Maendeleo *(Local Government Capital Development Grant)* ambayo Halmashauri inaweza kuzitumia kwa shughuli mbalimbali za maendeleo. Lakini jambo kubwa vilevile ni kuwa tathmini hii inatupa fursa ya kuwaelewa Viongozi na Watendaji, ambao ni kikwazo katika harakati zetu za kuwawezesha wananchi kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Spika, nauagiza Uongozi wa Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa, kuhakikisha kuwa taarifa ya zoezi hili inakamilishwa na kusambazwa kwa wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua kuwa katika mazingira ya dunia ya leo ya utandawazi na maendeleo makubwa yaliyofikiwa katika teknolojia ya habari na mawasiliano ya kisasa, nchi yetu ina changamoto kubwa ya kwenda kwa kasi zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani tena tuendelee na mbinu zile zile za uongozi wa kizamani. Tunahitajika kubadilika. Utawala na uongozi wetu nao lazima ubadilike. Tunahitajika tuwe wabunifu zaidi, tujitume zaidi, tuweke maslahi ya wananchi wetu mbele zaidi na tuibue hisia na ari ya wananchi wetu kupenda maendeleo na tamaa ya maisha bora.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ni lazima tujenge utamaduni wa kujifunza na kuiga mema yanayofanywa na wenzetu. Kila kiongozi anao wajibu mkubwa wa kuweka mkazo katika uwezeshaji na ushirikishwaji wa wananchi katika maendeleo.

Mfumo wa upimaji wa Halmashauri unatoa fursa ya kuamsha ari ya wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo yao kutokana na uelewa mpana wa programu na dhana ya utawala bora. Tutambue kuwa maisha bora kwa kila Mtanzania hayawezi kuletwa na Serikali pekee, yataletwa na wananchi wenyewe wakiwezeshwa na kushirikishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kuwahimiza Viongozi na Watendaji wote nchini kuzingatia mahitaji haya muhimu ya uongozi katika karne hii ya 21.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeazimia kwa dhati kuelekeza rasilimali zake nyingi pamoja na nguvu za uongozi na utaalam katika kuinua ubora wa elimu nchini, hii ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ya kuhakikisha kuwa hakuna mwanafunzi anayefaulu Elimu ya Msingi na kukosa nafasi ya kuingia Sekondari. *(Makofi)*

Kutokana na utekelezaji makini wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi *(MMEM),* Taifa limeshuhudia ongezeko kubwa la wanafunzi wa Shule za Msingi kutoka

4,382,410 mwaka 2000 hadi kufikia 7,959,884 mwaka 2006. Katika kipindi hicho hicho, kiwango cha kufaulu pia kimeongezeka kutoka asilimia 22 mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 70 mwaka 2006. Hili ni ongezeko la asilimia 48 kwa kipindi cha takribani miaka sita. Ni wazi kuwa kwa kasi hii, nchi yetu itafanikiwa kufikia utekelezaji wa lengo la pili la Malengo ya Maendeleo ya Milenia *(Millennium Development Goals)*, kabla ya muda uliowekwa wa mwaka 2015. Lengo hili linazitaka nchi zote wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wa kike na kiume wa rika lengwa wanaandikishwa na kumaliza Elimu ya Msingi. *(Makofi)*

Kasi ya Maendeleo yetu kwenye Shule za Msingi imewafurahisha hata washiriki wetu wa maendeleo. Kwa mfano, Mheshimiwa Hilary Benn, Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Uingereza akizungumza na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete Mwezi Januari, 2007 alikuwa na haya ya kusema, nami nanukuu: *'We often hear more about Africa's problems than we do about its progress. Yet across the Continent, democracy is growing, conflict has fallen and economic growith is strong. Tanzania is an excellent example of the progress Africa is making, with a constitutional democracy, economic growth above five percent a year and nearly all children in Primary Education."* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ongezeko la wanafunzi wanaofaulu Elimu ya Msingi ni kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaoingia Shule za Sekondari. Takwimu zinaonyesha kuwa uandikishaji wa wanafunzi katika Shule za Sekondari umeongezeka kutoka wanafunzi 99,744 mwaka 2003 hadi kufikia wanafunzi 243,359, mwaka 2006. Hata hivyo, changamoto kubwa ambayo Taifa linakabiliana nayo hivi sasa ni ongezeko kubwa la wanafunzi wanaofaulu Elimu ya Msingi na ambao hawana nafasi za kuwawezesha kujiunga na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa kwa mwaka 2006, jumla ya wanafunzi 467,997 walifaulu kwenda Sekondari. Kati ya idadi hiyo, wanafunzi waliochaguliwa katika awamu ya kwanza kujiunga na Sekondari ni 232,162, ikiwa ni sawa na asilimia 49.6 tu. Hii ina maana kuwa wanafunzi 235,835 ambao ni sawa na asilimia 50.4, hawakupata nafasi ya kujiunga na Sekondari katika awamu ya kwanza. Kiwango hiki ni kikubwa na kinasikitisha. Kinasikitisha kwa vile azma ya kijana mdogo wa Kitanzania mwenye nia ya kujiendeleza kielimu ni kuwezeshwa kufikia ukomo wa uwezo wake kielimu. Wazazi lazima watambue hilo, Halmashauri na Mikoa lazima itambue hilo na Taifa vile vile.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wanafunzi zaidi ya 397,959 sawa na asilimia 75 ya wote waliofaulu wanaingia Sekondari za Serikali ifikapo tarehe 15 Machi, mwaka 2007. Katika kuikabili hali hiyo, Serikali Kuu kwa kushirikiana na Uongozi wa Mikoa na Halmashauri imechukua hatua mbalimbali ambazo zitawezesha kujengwa kwa Shule mpya, kuongezwa kwa mikondo kwenye Shule za zamani, kujengwa kwa nyumba za Walimu na majengo mengine muhimu ya Shule, kununuliwa kwa samani na kupatikana kwa Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo methali ya kule Masaini, inasema: "Ugumu haupo katika kupata, bali katika kukilea na kukitunza." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamii zetu zielewe sasa kuwa tunajaliwa kuwapata watoto wengi jambo ambalo ni la faraja kwa kila familia, lakini vile vile kila familia itambue kuwa inao wajibu wa kushiriki kikamilifu katika kuwezesha watoto hawa kupata elimu ambayo ni haki yao ya msingi. Watanzania tukubali kuchangia elimu ya watoto wetu kwa kushiriki katika ujenzi wa Shule za Sekondari kama tunavyochangia harusi na sherehe nyingi nyingine. Naipongeza kwa dhati kabisa Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Dodoma ambayo ni kati ya Mikoa 10 iliyoshiriki katika Mikutano tuliyoitisha hivi karibuni. Mikoa hii imejiwekea mikakati itakayowawezesha kuwaingiza wanafunzi Sekondari kwa asilimia 100.

Narudia, wataingiza wanafunzi asilimia 100. Uzoefu umeonyesha kuwa mafanikio haya yanatokana na maandalizi mazuri na ya mapema na ushirikishwaji wa wananchi. Kwa mfano, kwa Mkoa wa Dodoma, kila mwananchi mwenye umri wa miaka 18 huchangia kiasi cha Sh. 5,000/= kwa ujenzi wa madarasa. Kwa utaratibu huu wa nguvu za wananchi, Mkoa uliweza kupata kiasi cha Shilingi bilioni 1.2 pamoja na vifaa mbalimbali yakiwemo mabati 7,456. Huu ni mfano mzuri sana wa kuigwa.

Nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa William Lukuvi pamoja na viongozi wenzake wa Mkoa wa Dodoma. Nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Dr. Jones Balele pamoja na Viongozi wa Mkoa wa Shinyanga. Kama wao wanaweza na sisi pia tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu Serikali ilioupata, Viongozi na Watendaji wa Mikoa na Halmashauri zake wanao wajibu wa kuchukua hatua za msingi zifuatazo:-

- Kuhahakikisha kwamba zaidi ya asilimia 75 ya Wanafunzi wa Darasa la Saba waliofaulu katika maeneo yao mwaka 2006 wanapata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza;

- Mikoa ambayo imeonekana kufanya vizuri, iongeze juhudi zaidi ili wanafunzi wote waliofaulu, asilimia 100 wapate nafasi ya kujiunga na Sekondari;

- Halmashauri zote zizingatie kuwa muda wa mwisho wa wanafunzi waliochaguliwa awamu ya pili kuanza masomo ni tarehe 15 Machi, 2007;

- Mikoa na Halmashauri zote zihakikishe zina mipango endelevu ya kusimamia kikamilifu ujenzi wa Shule na maendeleo ya elimu katika maeneo yao;

- Ujenzi wa Shule mpya, uzingatie ramani, viwango na maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kukidhi vigezo vinavyohitajika wakati wa usajili;

- Tujiandae vizuri kwa kuwafikisha vijana hawa Kidato cha Nne na tuanze sasa kuwatengenezea njia ya kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo mbalimbali vya Elimu ya Juu; na

- Wizara ya Elimu ihakikishe kwamba Walimu wapya wanapatikana ifikapo mwezi Machi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza vuguvugu hili la kuwaingiza watoto wengi waliofaulu Sekondari, Naibu Mawaziri wote watafanya ziara maalum kwenye Wilaya zote nchini kuanzia tarehe 15 mwezi Februari, 2007. Jukumu lao kubwa litakuwa ni kuhimiza utekelezaji wa maelekezo ya Serikali na kubadilishana uzoefu na viongozi wa Mikoa hiyo ili azma yetu itimie. Aidha, watatumia fursa hiyo kuendelea kuwahimiza wananchi kushiriki katika kuchangia utoaji wa elimu bora kwa watoto wetu na kuwezesha wanafunzi zaidi ya asilimia 75 kujiunga na Sekondari ifikapo tarehe 15 Machi kama nilivyokwishasema.

Watakuwepo vilevile wataalam watakaoungana na Naibu Mawaziri hawa katika ziara hizo. Timu hizo za wataalam zitajumuisha wataalam kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI*. Wote kwa pamoja watashiriki kutoa ushauri wa namna gani ya kuzisaidia Halmashauri kujipanga vizuri ili miaka ijayo zoezi la ujenzi wa Sekondari liwe endelevu. Kwa wale Waheshimiwa Wabunge watakaoweza, nitashukuru sana na nina hakika Manaibu Mawaziri watafurahi sana mkijiunga nao katika Majimbo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007, inakadiriwa kuwa wanafunzi watakaomaliza Elimu ya Shule za Msingi watafikia 800,000. Tukichukua asilimia 75 kama kiwango cha kufaulu, tutakuwa na wanafunzi 600,000 watakaohitaji nafasi za kujiunga na Elimu ya Sekondari. Hili ni ongezeko la asilimia 43.6. Kwa msingi huo, kila Mkuu wa Mkoa awasilishe Ofisi ya Waziri Mkuu - *TAMISEMI* taarifa yenye kuonyesha idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani ya Darasa la Saba mwaka, 2007 ifikapo tarehe 30 Mei, 2007. Aidha, taarifa hiyo ionyeshe makadirio ya wanaotarajiwa kufaulu, mipango na mikakati ya Mkoa kuwawezesha wote wanaofaulu kujiunga na Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika**,** tunasisitiza elimu kwa vile ndio msingi wa maendeleo ya nchi yetu. Ndio msingi wa kupata Taifa la watu wenye kufikiri, wenye mawazo mapya kila mara, wenye uwezo wa kutumia mabadiliko ya teknolojia na wenye utaalamu mbalimbali kwa faida ya nchi yetu. Tunataka Taifa letu liwe na wanafalsafa, wanasayansi na wanataaluma wengine wengi kwa vile wanao uelewa mpana wa mambo wanayokumbana nayo. Tuwawezeshe watoto wa Kitanzania kupata elimu hadi ukomo wa vipaji vyao ili Taifa liweze kunufaika kwa kutumia utaalamu wao kusaidiana na wananchi wenzao kuondoa kero na vikwazo vya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza tena Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya *TAMISEMI*, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanaosimamia suala hili la ujenzi wa Shule za Sekondari. Aidha, naipongeza Kamati ya Wabunge wa Hesabu za Serikali, chini ya Mheshimiwa Mgana Msindai, kwa kukagua shule hizo kila walikopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mengi nchini zimeleta neema na faraja kubwa sana kwa wakulima. Mvua hizi zikitumiwa vyema zitawawezesha wakulima kupata mavuno mazuri katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, yapo maeneo ambayo mvua hizi zimeanza kuwa nyingi kuliko inavyopasa na zimeanza kuathiri baadhi ya mazao. Kwa mfano, mvua zinazoendelea kunyesha hapa Dodoma zimeathiri mazao yaliyopandwa kwenye maeneo ya mabonde kwa vile hali ya unyevunyevu wa ardhi imekuwa kubwa na kusababisha maji kujaa kwenye mabonde hayo. Jukumu la viongozi na wataalam wa kilimo ni kuwawezesha wananchi wa maeneo kama hayo kukubali ushauri wa kutafuta maeneo mbadala na kupanda mazao yanayokomaa upesi ili kuweza kuzitumia mvua zinazoendelea kunyesha kabla ya mwisho wa msimu.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa msukumo wa kipekee katika Sekta ya Kilimo, mwezi Desemba mwaka 2006, Serikali ilifanya mapitio ya utekelezaji wa ahadi zake kwa wananchi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Mafanikio ya kuridhisha yamepatikana katika zoezi hilo. Lakini imebainika pia kuwa kuna changamoto nyingi za kukibadili kilimo chetu kuwa cha kisasa. Baadhi ya changamoto hizo ambazo Serikali inaandaa mikakati ya kuzishughulikia ni zifuatazo:-

- Kuutazama upya utaratibu uliopo wa uagizaji na usambazaji wa mbolea ili kutafuta utaratibu bora zaidi utakaowezesha mbolea kumfikia mkulima kwa bei ya chini; *(Makofi)*

- Kuandaa mkakati madhubuti wa kuimarisha huduma za ughani na utafiti;

- Kuendeleza utafiti katika Vyuo vya Utafiti vya Kilimo kwa kuviongezea uwezo ili viendeleze utafiti mkubwa na mzuri uliokwishafanywa na vilevile kuufikisha utafiti huo kwa wakulima. Kwa mfano, Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Lyamungu, nilichokitembelea Jumamosi iliyopita, kimefanikiwa kuzalisha aina mpya ya Kahawa Chotara yenye tija kubwa na ubora zaidi isiyoshambuliwa na magonjwa ya Chulebuni *(CBD)* ya kutu na majani. Nimeamua kutembelea Vituo vyote vya Utafiti wa Kilimo nchini ili kujua matatizo yao na jinsi vitakavyoshiriki zaidi katika kufufua kilimo; *(Makofi)*

- Kuweka mikakati ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji; na

- kuwezesha Sekta ya Ushirika nchini kukua kwa kasi zaidi kwani ndio mkombozi wa mkulima. Lakini kuwa na masoko ya uhakika kwa mazao ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mahsusi katika kukabiliana na changamoto hizi yanafanyiwa kazi na Wizara husika na yatakuwa sehemu ya mpango wa Serikali kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kama sote tulivyosikia ugonjwa wa homa ya Bonde la Ufa *(Rift Valley Fever)* umeingia nchini. Ugonjwa huu umeripotiwa kutokea Mkoani Arusha

tarehe 31 Januari, 2007, baada ya wagonjwa wawili kufariki katika Hospitali ya Mkoa ya Mount Meru Mjini Arusha. Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa unasababishwa na virusi ambavyo havina dawa na unaambukizwa kutokana na wadudu wanaowang'ata mifugo kama ngombe, mbuzi, nguruwe na kondoo. Dalili za ugonjwa kwa mifugo ni homa, mnyama kupunguza kula, kutokwa na makamasi na mate mengi. Dalili kwa upande wa binadamu ni pamoja na homa kali, maumivu ya viungo na misuli, kuharisha damu na kutokwa na damu puani.

Kutokana na kugundulika kwa ugonjwa huu, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

- Kusitisha mara moja usafirishaji wa mifugo kutoka eneo moja hadi lingine hasa Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro;

- Kuagiza dawa za chanjo nje ya nchi na kuchukua hatua za kuanza kuchanja mifugo. Gharama ya chanjo hizo ni Shilingi milioni 805; na

- Kuhakikisha mifugo yote inachinjwa kwenye machinjio yanayotambulika na Serikali na kuhakikisha Madaktari wanapima nyama hizo. Hakuna chanjo ya ugonjwa huu kwa binadamu isipokuwa dawa zipo kwa bakteria nyemelezi. Hivyo, wananchi wawahi kwenda Hospitali mara dalili zinapojitokeza.

Wito wangu kwa Viongozi wote kuanzia ngazi ya Tarafa, Wilaya na Mkoa ni kuhakikisha wananchi wanaelimishwa na kuhamasishwa kuhusu dalili na athari za ugonjwa huu na kuchukua tahadhari za kujikinga ikiwa ni pamoja na; wanasema moja ya tahadhari ni kutokula nyama au kunywa maziwa na wale wale ambao hawawezi kuvumilia sana kutokula nyama, basi ahakikishe nyama ile imeiva sana. Aidha, wazingatie maelekezo ya Madaktari wa mifugo ili tuweze kuzuia ugonjwa huu usienee nchini kwani ni hatari na unasababisha vifo mapema.

Mheshimiwa Spika, mpango wa uwezeshaji, tarehe 16 Agosti, mwaka 2006, katika hotuba yangu ya kuhitimisha Shughuli za Mkutano wa Nne wa Bunge la Bajeti, nilieleza utaratibu kuhusu mpango wa Serikali wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira nchini. Mpango huu ni ule wa kutoa wastani wa Shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa nchini kupitia taratibu za kibenki. Fedha hizi zinatolewa kama chachu ya kuwawezesha wajasiriamali kupata mikopo yenye masharti nafuu inayotolewa na Benki husika kupitia *SACCOS*, vikundi vinavyojishughulisha na uzalishaji mali au vya kibiashara na kwa wajasiriamali mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni pamoja na kukamilisha taratibu zinazohusika na kuwekeana Mikataba na Benki za *CRDB* na *NMB*. Kila Benki ya *CRDB* na *NMB* ilipokea Shilingi bilioni 5.25 mara baada ya Mikataba kusainiwa. Fedha ambazo zimetolewa kama dhamana. Aidha, kuanzia mwezi Novemba hadi Desemba mwaka 2006, Benki Kuu imetoa mafunzo kwa wataalam wapatao 1,050. Mafunzo hayo yamejumuisha Maafisa Mikopo wa Benki, Maafisa Ushirika, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Mipango Wilayani. Benki za *CRDB* na *NMB* zimetuma fedha kwenye Matawi yake Mikoani na mikopo imeanza kutolewa katika baadhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 8 Februari, Mikoa ambayo tayari ina maombi yanayoshughulikiwa katika hatua za mwisho ni Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kigoma, Lindi, Mbeya, Mtwara na Singida. Benki ya *CRDB* imepokea maombi yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.2 kutoka *SACCOS* nane zenye Wanachama 2,341.

Kati ya Vyama hivyo, Chama kimoja cha Manispaa ya Kinondoni chenye jumla ya Wanachama 220 kilipatiwa mkopo wa Shilingi Millioni 41. Vyama vingine ambavyo viko katika hatua za mwisho mwisho za kukamilisha taratibu ni pamoja na *Uso Mama SACCOS* (Babati); *Kipunguni SACCOS* (Ilala); *Meckbam SACCOS* (Babati); *Endasak SACCOS* (Hanang); *Mshikamano Magugu SACCOS* (Babati); *Igembe SACCOS* (Kahama) na *Sheb Mtola SACCOS* (Kahama). *(Makofi)*

Benki ya *NMB* nayo imepokea jumla ya maombi 1,300 yakiwemo maombi 1,289 ya mtu mmoja mmoja na maombi ya *SACCOS* 11. Jumla ya Shilingi Bilioni 2.9 zimeombwa na maombi yako katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kutoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizo, napenda kutoa wito na changamoto zifuatazo:-

(i) Viongozi wa *SACCOS* mbalimbali nchini waongeze kasi ya kuhamasisha wajasiriamali wake kuibua na kuandaa miradi mizuri inayokidhi vigezo vilivyowekwa na Benki, ili wajasiriamali wao waweze kunufaika na mikopo hii yenye masharti nafuu. Aidha, nahimiza *SACCOS* na vikundi mbalimbali vya ufundi kubuni miradi ya kutoa mikopo kwa njia ya kuwapa zana au pembejeo wajasiriamali wanaopenda kufanya hivyo, hasa wakulima Vijijini;

(ii) Maafisa mikopo wa Asasi za Kifedha waendelee kuwasaidia wajasiriamali mbalimbali na *SACCOS* ambazo ziliwasilisha miradi yenye mapungufu Benki, waweze kuiboresha na kukidhi vigezo vilivyowekwa ili kupata mikopo hiyo;

(iii) Viongozi wa Halmashauri zote nchini wawe na utaratibu maalum na endelevu utakaowawezesha wataalam wao waliopata mafunzo kwenda Vijijini kuwaelimisha wajasiriamali na wananchi kuibua na kuandaa miradi mizuri inayokidhi vigezo vya kibenki vya kupata mikopo hiyo; na

(iv) Kamati mbalimbali zilizoundwa kusimamia na kuratibu mpango huu katika ngazi zote zifuatilie kwa karibu utekelezaji wa zoezi hili. Aidha, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwekezaji na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ziimarishe uratibu na usimamizi wa mpango huu na kutoa taarifa mara ka mara na kuwaelimisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitumie fursa hii kuwahimiza Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwahamasisha Wapigakura wao katika Majimbo yao ili wajiunge pamoja kuanzisha Vikundi imara vya Kuweka na Kukopa. Lengo letu ni kujenga jeshi imara la wajasiriamali nchini. Tumeanza vizuri, tusirudi nyuma ila tuongeze kasi. Ni matumaini yangu kuwa tukiendelea na ushirikiano huu tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, masuala ya kimataifa, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilimaliza kipindi chake cha uanachama wa miaka miwili wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuanzia tarehe 01 Januari, 2005 hadi tarehe 31 Desemba, 2006. Wakati wa Uanachama wa nchi yetu, Tanzania ilipata fursa ya kuwa Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa Mwezi Januari, 2006.

Katika kipindi chetu cha Urais, tuliandaa majadiliano ya wazi ya Mawaziri kuhusu masuala ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu. Kutokana na majadiliano hayo, tuliweza kuharakisha kufanyika kwa Mkutano wa Pili wa Umoja wa Mataifa wa Nchi za Maziwa Makuu Mjini Nairobi, Kenya, tarehe 14 hadi 15 Desemba, 2006. Mkutano huo, pamoja na mambo mengine, ulimchagua Katibu Mtendaji wa kwanza wa Sekretarieti ya Nchi za Ukanda Maziwa Makuu kutoka Tanzania na kama kawaida yetu ni mwanamke. Tunaonyesha mfano Afrika, Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, napenda kumpongeza kwa kuchaguliwa kwake kushika wadhifa huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa hasa ilipokuwa chini ya Uongozi wa Dr. Asha-Rose Migiro maana yake ndiye aliyeyafanya haya na haya Ubalozi wetu wa Kudumu wa Umoja wa Taifa *New York* chini ya Waheshimiwa Mabalozi Augustine Mahiga na Tuvako Manongi kwa kazi nzuri ya kuliweka jina la nchi yetu kwenye ramani ya dunia. Napenda kuwapongeza Mabalozi hawa kwa kazi yao nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha hoja yangu, napenda kusisitiza maeneo muhimu yafuatayo:-

(i) Utendaji katika Halmashauri bado unahitaji msukumo mkubwa ili kufikia vigezo na malengo tuliyojiwekea katika utendaji wa shughuli za Serikali;

Pamoja na kuzipongeza Halmashauri zilizopata alama nzuri katika tathmini iliyofanywa kuhusu utawala bora, Halmashauri zilizofanya vibaya zinatakiwa ziongeze juhudi na kufikia vigezo vilivyowekwa kwa haraka na kwa kasi inayopasa;

(ii) Mafanikio katika Sekta ya Elimu yanaonekana ni dhahiri na ya kujivunia. Lakini napenda kusisitiza tuendelee kwa ari na kasi hii hii ili tuweze kuwawezesha watoto wetu wengi kupata haki yao ya msingi ya elimu;

(iii) Bado tuna kazi kubwa ya kuboresha na kuendeleza kilimo chetu kiwe cha kisasa, chenye tija kubwa na cha kibiashara. Tuweke juhudi zaidi katika kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha kutumia wanyamakazi na matrekta. Tuhimize matumizi ya mbegu bora na mbolea ili kuongeza uzalishaji; na

(iv) Tunayo nafasi nzuri ya matumizi ya Mfuko wa Uwezeshaji. Tutumie nafasi hii kuibua miradi itakayokubalika katika mabenki ili watu waweze kupata mikopo kwa kutumia fursa zilizopo na kujiletea maisha bora.

Mheshimiwa Spika, mara zote tunapofikia mwisho wa shughuli ya Mkutano wa Bunge kama huu, tunakuwa na kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda hadi sasa. Aidha, tunayo sababu za msingi za kuwashukuru wote walioshiriki katika kutoa huduma muhimu na hatimaye kufanikisha Mkutano wetu huu.

Shukrani za pekee ni kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kwa *standard* na *speed* kwa busara na uthabiti kukamilisha vikao vyote vilivyopangwa. Nakupongeza sana. Aidha, namshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi zao nzuri. Niruhusu pia nimshukuru Katibu wa Bunge Bwana Damian Foka na Wasaidizi wake wote kwa kutuwezesha kufanya kazi hii vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati ninatoa hoja ya kufunga Mkutano wa Tano wa Bunge lako Tukufu tulimwomba Mwenyezi Mungu atujalie sote tuweze kumaliza salama mwaka 2006. Tunao wajibu wa kumshukuru kwa yote. Wapo wananchi wenzetu wengi ambao hawakupewa fursa ya kuuona mwaka 2007; lakini wengi wetu tumeuona. Tutumie basi fursa tuliyopewa na Mwenyezi Mungu kujibidisha ili tupige hatua zaidi mbele na hasa maendeleo ya watu wetu. Leo tunaagana hapa tukiwa na malengo ya kutekeleza na kuyakamilisha katika mwaka mpya wa 2007.

Napenda kusisitiza umuhimu wa kila mmoja wetu kutimiza wajibu wake katika kutekeleza malengo tuliyojiwekea ya kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi wetu. Nawatakieni nyote safari njema ya kurejea Majimboni mwenu na katika Vituo vyenu vya Kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa hadi tarehe 10 Aprili, 2007, saa 3.00 asubuhi litakapokutana hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hoja hiyo nzito.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijawahoji. Ninalo tangazo. Mheshimiwa Masilingi - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, ameniomba nitangaze kwamba Kamati hiyo itakutana mara baada ya kuahirishwa Bunge, Chumba Na. 231.

Waheshimiwa Wabunge hoja iliyoko mbele yetu ni ya kuliahirisha Bunge na imeungwa mkono. Sasa nawatangazia huku nikiwatakia safari njema kwamba naliahirisha Bunge hadi siku ya Jumanne tarehe 10 Aprili mwaka huu wa 2007 saa Tatu Asubuhi, hapa Mjini Dodoma. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 05.57 mchana Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 10 Aprili, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*